**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI-OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO

**DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM)**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Juni, 2024**



***"Ni matamanio yangu kuyadumisha Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuyatafsiri katika muktadha na mahitaji ya sasa ambayo ni ukombozi wa kiuchumi"***

Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

**Ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi 11 Novemba 2020.**

## YALIYOMO


A. UTANGULIZI ..... 1
B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI 2023-MACHI 2024 . 5
B.1 Mapato ya Serikali Julai-Machi 2023/2024 ..... 5
a. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ..... 6
b. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar ..... 6
c. Mapato ya Wafanyakazi wa SMT walioko Zanzibar ..... 6
d. Mapato yasiyokuwa ya Kodi ..... 6
e. Mapato kwa ajili ya Mfuko wa Miundombinu ..... 7
f. Mapato ya Mfuko wa Barabara ..... 7
g. Mkopo wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kupitia utaratibu wa mkopo wa ndani ..... 7
h. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ..... 8
i. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ..... 9
B.2 Matumizi ya Serikali Julai-Machi 2023/2024 ..... 9
a) Matumizi ya Kawaida ..... 9
b) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ..... 11
C. MISAMAHA YA KODI ILIYOTOLEWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024 ..... 12
D. DENI LA TAIFA ..... 13
Mwenendo wa Deni la Taifa ..... 13
E. UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA SERA ZA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024 ..... 14
E.1 Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya Mwaka 1998 ..... 14
E.2 Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali Nam. 11 ya Mwaka 2008 ..... 16
E.3 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015 ..... 17
E.5 Marekebisho katika Sheria ya Tozo la Petroli Nam.7 ya Mwaka 2001 ..... 18
F. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024. ..... 19
G. CHANGAMOTO UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI 2024 ..... 49
H. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI 2023 HADI JUNI 2024 ..... 50

I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024.................. 53
- Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi jumuishi mwaka 2024/2025. ........................................................... 53
- Uchumi wa Kidijitali (Digital economy) ....................................... 55
- Zanzibar na Uchumi wa kidijitali .............................................. 56

J. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.............................................................. 56
K. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2024/2025............................................................................ 57
i. Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato .......................................... 64
ii. Mapendekezo ya Mgao wa Matumizi.......................................... 68
L. VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.... 69
M. MAGEUZI YA BAJETI INAYOZINGATIA JINSIA NA USAWA............ 75
N. UGHARAMIAJI WA NAKISI YA BAJETI......................................... 76
O. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2024/2025............................ 77
P. MAZINGATIO YA MAENEO MAHSUSI KWA BAJETI YA 2024/2025.. 77
Q. SHUKURANI ........................................................................ 78
R. HITIMISHO............................................................................ 82
S. VIAMBATISHO......................................................................... 83

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, hatuna budi kumshukuru Allah Subhanahu Wataala kwa kuendelea kutupa neema yake ya pumzi na afya njema sambamba na kutubarikia upendo na mshikamano miongoni mwetu na Taifa kwa ujumla. Kwa hakika Allah ameturuzuku neema ya amani na utulivu katika visiwa vyetu.

2. **Mheshimiwa Spika,** Mbele yako na Baraza lako Tukufu, nimesimama kutimiza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 105 kinachomtaka Waziri anayehusika na fedha kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi, **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka Unaofuata.** Kwa mantiki hiyo, naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako sasa likae kama Kamati kwa ajili ya kujadili, kushauri na hatimae kuidhinisha **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inaendelea na mkakati wa kuibadilisha taswira ya Zanzibar kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati; maeneo ya uzalishaji; kugharamia utoaji wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya, elimu, maji na umeme; sambamba na kuimarisha sekta za utalii na uwekezaji kwa lengo la kuinua kipato cha mwananchi na uchumi wa Zanzibar kwa ujumla wake.

4. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi, kwa uchache na kwa unyenyekevu naomba nitoe shukurani zangu za moyoni kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia maendeleo ya nchi yetu kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ukweli nikisema nitoe pongezi nitamaliza muda wote wa hotuba yangu na nitakuwa nikirudia yale ambayo wananchi wanayajua. Itoshe tu kusema kuwa mwangaza wa matumaini kwa wazanzibari umeanza kuonekana, na mshumaa wa maendeleo unaendelea kumurika ndani na nje ya visiwa vyetu na kutoa mwanga wa mafanikio.

5. **Mheshimiwa Spika,** Simulizi juu ya mageuzi yetu ya kijamii na kiuchumi inahusisha **Safari Ndefu ya Mafanikio yaliyopatikana kwa Muda Mfupi.** Hadithi hiyo ilianzia kusimulia mabati, tukaendelea na simulizi za maghorofa ya skuli, hospitali, masoko ya kisasa, barabara, stendi za magari, viwanja vya michezo na haikuacha kutuhabarisha juu ya maslahi ya watumishi wa umma, wastaafu, pamoja na ajira za vijana. Masikio ya wazanzibari, watanzania na Dunia kwa ujumla wanasikia na kwa macho yao wanaona.

6. **Mheshimiwa Spika,** Ndoto ya ukweli ya safari yetu kwa imani na ithibati, kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ni Muungwana na anatuthibitishia kwa vitendo msemo na maana halisi ya **"Ada ya Mja Hunena Muungwana ni Vitendo".** Anasema, tunasikia na anatenda, tunaona. ***Kwa sasa tunaendelea na simulizi ya maandalizi ya usafiri wa taxi za baharini na bado tunaendelea na makubwa zaidi..................!!!!! Miaka mitatu imetosha kwa wananchi kuipima Serikali inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi mkuu ujao.***

7. **Mheshimiwa Spika,** Sisi viongozi ni mashahidi na mashuhuda wa kuweza kusimulia hadithi za mafanikio kwa mifano hai iliyopo. Leo hii, tuna kila sababu ya kusema mustakabali wa Maendeleo na Uchumi wa Zanzibar umekuwa, na sina shaka mnakubaliana nami mshikamano na umadhubuti wa mizizi hupelekea Ustawi na Uimara wa Matawi. Hii inamaanisha kuwa nguzo ya uongozi ni wasaidizi imara wanaojitolea na kujituma kwa nia na dhamira njema ya nchi yao. Hivyo kipekee nawapongeza wasaidizi wa Mheshimiwa Rais wakiwemo; Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa, **Othman Masoud Othman**, Makamo wa Pili wa Rais, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote bila kusahau viongozi wote wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, kwa jitihada zao na maarifa katika harakati za kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu na kufanikisha ahadi alizozitoa kwa wananchi.

8. **Mheshimiwa Spika,** Hakika mapendekezo, ushauri, na miongozo mliyoitoa kupitia Kamati na vikao mbali mbali yamewezesha kufikia mafanikio makubwa katika matayarisho ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbali mbali na Serikali. Kwa kiasi kikubwa maoni yenu yamesaidia kuikamilisha bajeti hii kwa ufanisi na kutuwezesha kusimama hapa leo tukitimiza wajibu huu muhimu kwa Taifa letu. Hivyo basi, niruhusu nitoe shukurani na pongezi zangu za kipekee kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi **Zubeir Ali Maulid** na Wasaidizi wako wote wakiwemo Mheshimiwa Naibu Spika; Wenyeviti wa Baraza pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Hii inathibitisha kauli ya Mhe. Rais wakati wa ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi Novemba 11, 2020 naomba nimnukuu ***"Mimi naamini kuwa Baraza la Wawakilishi imara huzaa Serikali imara".***

9. **Mheshimiwa Spika,** Kipekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti wakiongozwa na Mwenyekiti **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma** kwa mashirikiano, miongozo na kujitolea kwao kuhakikisha mipango tuliyojipangia na kuidhinishiwa na Baraza letu hili inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, usalama, amani, utulivu na maendeleo yake unategemea sana uhusiano imara uliokuwepo. Kiukweli tunajivunia uwepo na faida za muungano huu na tunamshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nidhahiri kuwa, mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, nafasi ya mama inamchango mkubwa na ni alama ya kielelezo cha uwepo wake kwa wazanzibari, napenda pia kuwashukuru Makamu wake **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango** na **Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa** kwa nia yao ya dhati ya kuleta maendeleo na mashirikiano mazuri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

11. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuifanyia kazi kwa vitendo **Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** alipokuwa akizindua Baraza hili la Kumi la Wawakilishi tarehe 11 Novemba 2020. Katika hotuba ile, Mheshimiwa Rais alibainisha na kusisitiza maeneo yote ambayo kimsingi Serikali ina jukumu la kuyatekeleza. **Nina fahari kubwa sana kutangaza kwamba kwa kiasi kikubwa kuwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais tayari yameshatekelezwa kwa mafanikio makubwa na mengine yanaendelea kutekelezwa na yanatarajiwa kuendelea katika bajeti hii ya Mwaka 2024/2025.**

12. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais alitoa tamko la ahadi 51 ambazo zimegusa moja kwa moja sekta za jamii. Miongoni mwa mafanikio hayo kwa mujibu wa tathmini ya kina iliyofanyika kupitia sekta sita za kijamii, hadi kufikia Machi 2024, asilimia 96 zimeshafanyiwa kazi ambapo kati ya hizo; asilimia 55 zimekamilika, asilimia 41 zinaendelea kutekelezwa na asilimia 4 tu hazijaanza kufanyiwa kazi.

13. **Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe mafanikio haya yamelenga maeneo yale tu yaliyoainishwa katika ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi kiukweli yapo mengine yametekelezwa ziada ya hayo, sekta hizo zinahusisha;
    i. Sekta ya afya imefanikiwa kwa asilimia 70 kwa mujibu wa yaliyoahidiwa;
    ii. Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imefanikiwa kwa asilimia 67;
    iii. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanikiwa asilimia 60;
    iv. Sekta ya Maji na Nishati imefanikiwa asilimia 57 ya ahadi zilizotolewa;
    v. Uchumi wa Buluu imefanikiwa asilimia 50; na
    vi. Kilimo asilimia 40.

14. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa matamko hayo ni kuimarika kwa upatikanaji wa vifaa tiba kwa kuongeza bajeti, kuongeza bajeti ya sekta ya elimu, kuongeza kiwango cha pencheni, kuboresha miundombinu ya maji, na kusaidia kilimo cha mwani n.k.

## B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024

15. **Mheshimiwa Spika,** Nikiwa nawasilisha **Tathmini ya Utekelezaji wa Mapato na Matumizi ya Serikali** naomba tuweke mazingatio na taarifa za **Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar** ambazo nimeziwasilisha asubuhi ya leo kuwa ni sehemu ya hotuba hii.

16. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia **TZS 2,840.85 bilioni.** Kati ya fedha hizo, **TZS 2,822.85 bilioni** ni kwa upande wa Serikali Kuu na **TZS 18.00 bilioni** ni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### B.1 Mapato ya Serikali

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2023/2024, Serikali imefanikiwa kukusanya **TZS 2,216.51 bilioni** sawa na **asilimia 78** ya malengo ya kukusanya **TZS 2,840.85 bilioni** kwa mwaka, na **asilimia 100.5** kwa makadirio ya Julai-Machi 2023/2024 ya kukusanya **TZS 2,203.10 bilioni.** Mapato yaliyokusanywa katika kipindi cha tathmini yameonesha ukuaji wa **asilimia 99**, ikilinganishwa na mapato ya **TZS 1,110.65 bilioni** yaliyokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023.

18. **Mheshimiwa Spika,** Ongezeko hilo linatokana na sababu zifuatazo;
    i. Kupatikana kwa mapato yaliyotokana na Mikopo ya Hati Fungani na Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo.
    ii. Kuongezeka kwa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

iii. Kuongezeka kwa makusanyo ya kodi katika kipindi cha miezi tisa mwaka 2023/2024 ukilinganisha na kipindi cha miezi tisa mwaka 2022/2023.

### a. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

**19.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2023/2024, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imekadiriwa kukusanya **TZS 675.60 bilioni.** Hadi kufikia Machi 2024, Mamlaka imekusanya **TZS 559.34 bilioni** sawa na **asilimia 82.8** ya lengo la mwaka na ni sawa na **asilimia 104.4** kwa makadirio ya kukusanya **TZS 535.71 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Hii ni sawa na ukuaji wa **asilimia 24.5** ikilinganishwa na **TZS 449.26 bilioni** zilizokusanywa katika kipindi cha tathmini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### b. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, TRA kwa upande wa Zanzibar imekusanya **TZS 373.17 bilioni** sawa na **asilimia 71.7** ya bajeti ya mwaka ya **TZS 520.64 bilioni** na **asilimia 96.5** kwa makadirio ya kipindi cha tathmini ya **TZS 368.53 bilioni.** Mapato yaliyokusanywa yameonesha ukuaji wa **asilimia 15.5** ikilinganishwa na **TZS 323.01 bilioni** zilizokusanywa kwa kipindi kama hichi mwaka 2022/2023.

### c. Mapato ya Wafanyakazi wa SMT walioko Zanzibar

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Kodi ya wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walioko Zanzibar makusanyo halisi ni **TZS 15.75 bilioni,** sawa na **asilimia 100** ya makadirio ya kipindi cha tathmini.

### d. Mapato yasiyokuwa ya Kodi

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi kwa kipindi cha miezi tisa yamefikia **TZS 127.63 bilioni** sawa na **asilimia 63.2**

ya bajeti ya mwaka ya **TZS 201.79 bilioni** na **asilimia 78.9** kwa kipindi cha tathmini. Mapato hayo yanajumuisha; mapato yanayotokana na makusanyo ya Wizara na Taasisi za Serikali ya **TZS 122.98 bilioni,** Gawio la Benki Kuu ya Tanzania la **TZS 4.5 bilioni na TZS 150** milioni gawio kutoka Shirika la Bima Zanzibar (ZIC). Mapato hayo yanaonesha ukuaji wa **asilimia 9.7** ukilinganisha na mapato ya **TZS 116.3 bilioni** zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023.

### e. Mapato kwa ajili ya Mfuko wa Miundombinu

**23. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 Machi 2024, Serikali imekusanya **TZS 54.22 bilioni** kutoka Mfuko wa Miundombinu sawa na asilimia 218 ya makadirio ya kukusanya **TZS 24.87 bilioni** kwa mwaka 2023/2024. Kati ya makusanyo hayo TZS 51.09 bilioni yamekusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na **TZS 3.13 bilioni** zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar. Miongoni mwa sababu ya kuongezeka kwa kodi hiyo ni kutokana na hatua zinazochukuliwa za kuongeza viwango vya utozaji kodi ya miundombinu kutoka Dola Moja ya Marekani kwa kiwango cha awali na kufikia Dola 2 hadi Dola 5 kulingana na hadhi ya hoteli kwa mgeni anayelala katika hoteli na nyumba za kulala wageni za Zanzibar.

### f. Mapato ya Mfuko wa Barabara

**24. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Barababara una lengo la kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya matengenezo na kuimarisha miundombinu ya barabara. Kwa kipindi cha miezi tisa, Mfuko ulikusanya TZS 13.88 bilioni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya TZS 14.3 bilioni kwa kipindi cha tathmini na asilimia 57 kwa makadirio ya TZS 24.18 bilioni kwa mwaka.

### g. Mkopo wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kupitia utaratibu wa mkopo wa ndani

25. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imepanga kukopa TZS 717 bilioni ikiwa ni mikopo kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kupitia Mikopo ya Hati Fungani ya TZS 150 bilioni na Mikopo ya Kibiashara TZS 567.21 bilioni. Hadi kukamilika kwa robo ya tatu, kiasi cha TZS 596.63 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 94.6 ya kipindi cha tathmini na asilimia 83.2 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo Hati Fungani ni TZS 108.84 bilioni na Mikopo ya Kibiashara kutoka Benki za NBC na NMB ni T**ZS 487.79 bilioni.**

### h. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

26. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai - Machi 2023/2024 Serikali ilitarajia kupokea **TZS 459.70 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Fedha halisi zilizopokelewa ni **TZS 534.83 bilioni** sawa na **asilimia 116.3** kwa kipindi cha tathmini na **asilimia 77.9** ya makadirio ya mwaka ya **TZS 686.61 bilioni.** Mapato yaliyokusanywa yameongezeka kwa **asilimia 196** ikilinganishwa na **TZS 180.49** bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho **Mwaka wa Fedha 2022/2023.** Fedha hizo zimepatikana katika maeneo yafuatayo:

i. **Mikopo Nafuu ya Miradi ya Kisekta**
**TZS 404.15 bilioni** sawa na **asilimia 76.4** ya bajeti ya mwaka na **asilimia 129** kwa kipindi cha miezi tisa zimepatikana. Mkopo huo uliopatikana unaonesha ukuaji wa **asilimia 404** ukilinganishwa na mkopo wa **TZS 80.14 bilioni** uliopatikana kwa kipindi kama hichi mwaka 2022/2023.

ii. **Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**
Fedha zilizopatikana ni **TZS 57.47 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi mbali mbali. Hii ni sawa na **asilimia 54.8** ya bajeti ya mwaka na **asilimia 60** kwa kipindi cha miezi tisa.

iii. **Misaada ya Kibajeti**
**TZS 72.9 bilioni,** zinatokana na Misaada ya Kibajeti (General Budget Support) sawa na **asilimia 139.8** ya bajeti ya mwaka na **asilimia 140.3** kwa kipindi cha miezi tisa.

iv. **Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo (Basket Fund)**
**TZS 240 milioni** zimepatikana kutoka Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo, ambazo ni sawa na **asilimia 100** ya makadirio ya mwaka.

i. **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**27. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, makusanyo yamefikia **TZS 9.17 bilioni** sawa na **asilimia 72** ya makadirio ya kukusanya **TZS 12.72 bilioni** ya makadirio ya kipindi cha tathmini sawa na **asilimia 50.94** ya makadirio ya mwaka.

**B.2 Matumizi ya Serikali Julai-Machi 2023/2024**

**28. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2023/2024, matumizi halisi yalifikia **TZS 2, 2119.23 bilioni,** sawa na **asilimia 78.12** ya makadirio ya bajeti ya mwaka ya **TZS 2,840.85 bilioni** na **asilimia 111.6** ya makadirio ya **TZS 1,988.26 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Matumizi haya yamejumuisha kazi zifuatazo;

a) **Matumizi ya Kazi za Kawaida**

**29. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi 2023/2024), **TZS 919.74 bilioni** zimetumika kwa matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 69.74** ya kutumia **TZS 1,318.86 bilioni** kwa mwaka na **asilimia 96** kwa makadirio ya **TZS 958.79 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimetumika kwa kazi za kawaida kwa ufafanuzi ufuatao:

i. Mishahara kwa Mafungu ya Bajeti na Taasisi zinazopokea Ruzuku, **TZS 513.07 bilioni** sawa na asilimia 99.9 ya makadirio ya **TZS 515.89 bilioni** kwa kipindi hicho.
ii. **TZS 187.33 bilioni** zilitumika katika matumizi mengineyo ya Mafungu na Taasisi zinazopokea Ruzuku sawa na asilimia 77.8 ya makadirio ya **TZS 240.86 bilioni,** kwa kipindi cha tathmini.

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali ni **TZS 214.96 bilioni** sawa na asilimia 106 ya makadirio ya kutumia **TZS 202.04 bilioni** katika kipindi hicho na asilimia 84 kwa bajeti ya **TZS 256.00** bilioni kwa mwaka. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:
   a. Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo **TZS 24.99 bilioni** kwa wastaafu 1,240 wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;
   b. Malipo ya Pencheni kwa Wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni TZS 34.10 bilioni kwa wastaafu 13,795;
   c. Malipo ya Pencheni Jamii TZS 13.84 bilioni kwa wastani wa wazee 30,112 wa Zanzibar;
   d. Matumizi mengineyo ya Serikali ni TZS 72.71 bilioni; na
   e. Malipo ya riba ya Hati Fungani na mikopo ya ndani TZS 69.31 bilioni.

### 01.Malipo ya Deni na Dhamana za Serikali

30. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi, 2023/2024, Serikali ililipa Deni la Riba ya Hati Fungani na Mikopo ya Ndani ya **TZS 69.31 bilioni** ambayo inajumuisha:
   i. Malipo ya marejesho ya mkopo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii TZS 5.63 bilioni;
   ii. Malipo na Riba ya Hati Fungani na Mtaji TZS 39.54 bilioni; na
   iii. Malipo ya riba mkopo wa Benki ya Watu wa Zanzibar na Benki ya NBC TZS 24.13 bilioni.

### 02.Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

31. **Mheshimiwa Spika, TZS 10.8 bilioni** zilipangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Machi, 2024 matumizi halisi yamefikia TZS 4.39 bilioni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya mwaka na asilimia 54.9 ya makadirio ya TZS 8 bilioni ya kipindi hicho.

**b) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo**

**32.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Machi 31, 2024 matumizi halisi yalifikia **TZS 1,299.34 bilioni** ambapo **TZS 1,297.91 bilion**i kutoka Serikali kuu (TZS 836.5 bilioni kutoka Serikalini, **TZS 461.62 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambayo imejumuisha Mikopo nafuu ya kisekta **TZS 404.15 bilioni** na TZS 57.47 bilioni ni Misaada) na **TZS 1.58 bilioni** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**01.Mfuko wa Kuhudumia Madeni (Debt Service Fund)**

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa kiasi cha **TZS 273.44 bilioni** zimewekwa katika mfuko wa kuhudumia madeni sawa na asilimia 189.9 ya makadirio ya mwaka. Kiwango hicho kikubwa kuliko makadirio ya awali ni kutokana na mkakati wa Serikali wa kuendelea kukopa na kupata fursa za kukopa kutokana na akiba iliyojiwekea kama dhamana ya mikopo hiyo.

**02. Matumizi ya Mfuko wa Barabara**

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, fedha zilizotumika kupitia Mfuko wa Barabara ni **TZS 8 bilioni.** Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kazi za utunzaji na matengenezo ya barabara za Unguja na Pemba zilizopangwa kupatiwa fedha kutoka Mfuko huo.

**03.Mfuko wa Ustahamilivu wa Bei (Price Stabilization Fund)**

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu ulipangiwa kuchangiwa na mashirika mbali mbali kutokana na vianzio vyao vya mapato. Changamoto iliyokuwepo kuwa bado kuna muitiko mdogo wa taasisi zilizopangiwa kuchangia mfuko huo. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itakamilisha utaratibu maalumu kwa Taasisi zinazotakiwa kuchangia na Mashirika

ili ziweze kuchangia kwa mujibu wa uwezo wa Taasisi husika. Miongoni mwa hatua ambazo zitachukuliwa ni pamoja na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wao kupitia taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hadi Machi 2024, **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA)** pekee ndio imechangia kwa kiasi cha **TZS TZS 3.2 bilioni** ikiwa ni asilimia 15 ya mapato anayokusanya.

### 04. Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

36. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, TZS 1.58 bilioni zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 39 ya makadirio ya kutumia TZS 4 bilioni kwa kipindi cha tathmini.

## C. MISAMAHA YA KODI ILIYOTOLEWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi, 2023/2024, maombi 265 ya misamaha ya kodi kutoka taasisi za umma, wawekezaji, miradi ya maendeleo na watu binafsi yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, maombi 187 yamekubaliwa kutokana na kukidhi masharti ya sheria na maombi 33 yamekataliwa. Aidha, maombi ya misamaha 45 iliyobakia haikukidhi utaratibu wa maombi ya misamaha ikiwemo kutokamilika kwa baadhi ya taarifa za maombi pamoja na kutokamilika kwa taratibu za ufuatiliaji wa maombi hayo.

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hicho, misamaha yote iliyotolewa ilikuwa na thamani ya TZS 66.41 bilioni. Kumekuwa na ongezeko la misamaha ya kodi ukilinganisha na misamaha ya TZS 65.7 bilioni iliyotolewa katika kipindi kama hichi mwaka 2022/2023 kutokana na kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inapata misamaha kwa mujibu wa sheria.

## D. DENI LA TAIFA

### Mwenendo wa Deni la Taifa

39. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, hukopa ili kuweza kufidia nakisi ya bajeti kwa ajili ya kuendeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Utaratibu huu huiwezesha Serikali kutekeleza miradi hiyo na kurudisha mikopo hiyo kidogo kidogo. Pia Serikali imepanga utaratibu maalumu wa ulipaji wa deni husika pamoja na gharama zake bila ya kuathiri shughuli za kiuchumi.

40. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi wa Machi 2024, Serikali ina jumla ya Deni la Ndani **TZS 1,105.080 bilioni** kati ya Deni hilo Hati Fungani za muda mrefu ni **TZS 373.89 bilioni;** Deni kutoka taasisi za kifedha ni **TZS 545.46 bilioni;** na dhamana za Serikali kwa taasisi mbali mbali ni **TZS 185.72 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

41. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Thamani ya Sasa ya Deni (Present Value) ni TZS 1,052.46 bilioni. Tathmini ya Uwiano wa Deni la Taifa kwa ukuaji wa Uchumi kwa thamani halisi kwa kutumia Pato la Taifa "GDP at Constant Price" ya TZS 3,758.6 bilioni limefikia kiwango cha asilimia 28. Aidha, kwa kutumia "GDP at Current Price" ya TZS 6,041.6 bilioni. Tathmini ya Uwiano wa Deni la Taifa kwa ukuaji wa uchumi kwa thamani halisi limefikia kiwango cha asilimia 17.4, ambapo uwiano unaokubalika kwa nchi zenye uchumi mdogo wa kati kama Tanzania na Zanzibar usizidi asilimia 55. Kwa kutumia vipimo vyote viwili, tathmini ya Deni la Taifa inaonyesha kuwa bado ni himilivu na Serikali itaendelea kukopa ili kutekeleza miradi ya maendeleo yenye kuleta tija ya kiuchumi na uzalishaji.

42. **Mheshimiwa Spika**, Vile vile dhamana zinakuwa ni sehemu ya Deni la Taifa. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imetoa dhamana ya TZS 120.61 bilioni kwa Taasisi zifuatazo:

i. Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) TZS 65.93 bilioni,
ii. Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) TZS 10.00 bilioni,
iii. Kampuni ya Mwani (ZASCO) TZS 12.5 bilioni,
iv. Manispaa ya Magharibi "A' TZS 830 milioni,
v. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) TZS 17.85 bilioni,
vi. Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui (Z-MUX) TZS 4.5 bilioni, na
vii. Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) TZS 9.0 bilioni.

## E. UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA SERA ZA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024

**43. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24, Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Hatua hizo zilihusisha marekebisho ya Sheria pamoja na Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi.

**Muhtasari wa utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo;-**

### E.1 Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya Mwaka 1998

**i. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Uuzaji wa Nyumba Nafuu (Affordable Housing Scheme)**

**44. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali kwa kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Miradi ya Nyumba Nafuu (Affordable Housing Scheme) ili kuimarisha makaazi bora kwa wananchi pamoja na kupunguza gharama za ununuzi wa nyumba hizo. Hadi kufikia Machi, 2024, miradi miwili imenufaika na unafuu huo ikiwemo; Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Bei Nafuu katika Mji wa Dkt. Hussein Mwinyi eneo la Uwanja wa Magereza, wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Mradi wa Nyumba za Makaazi Mombasa unaojengwa

na Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC). Kiasi cha TZS 5.5 bilioni zimepatikana kwa kuuzwa nyumba zote 72 katika Mradi wa Nyumba kupitia Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC) uliopo kwa Mchina na nyumba 87 za ZSSF kwa kiasi cha TZS 5.08 bilioni tayari zimeuzwa.

**ii. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wakati wa Uingizaji wa Ndege, Injini za ndege, Vipuri na huduma za matengenezo zinazofanyika nchini**

**45. Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji wa Ndege, Injini za Ndege, Vipuri pamoja na huduma za matengenezo ili kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuongeza ujuzi wa huduma za ufundi wa ndege nchini. Utekelezaji wa hatua hiyo umeanza rasmi Julai, 2023.

**iii. Kupunguza unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Asasi za Kiraia kutoka asilimia 75 hadi asilimia 50**

**46. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kupunguza unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Asasi za Kiraia (NGO's & CSO's) pamoja na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa kazi kwa kipindi cha miaka miwili na vyanzo vya mapato kutoka ndani na nje ya nchi ili kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi pamoja na kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi, 2024 Jumla ya TZS 3.08 bilioni zimeokolewa kutokana na hatua hii.

**iv. Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa "Green House" na vifaa vyake**

**47. Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa lengo la kuimarisha shughuli za kilimo cha kisasa, kuongeza uzalishaji, kupunguza uagizaji wa chakula kutoka nje pamoja na kupunguza mfumko wa bei nchini. Utekelezaji hatua hiyo umeanza rasmi Julai, 2023.

v. **Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa Vifaa vya Umeme Unaotokana na Nishati Jadidifu (Renewable Energy)**

48. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali la kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji wa Vifaa vya Umeme Unaotokana na Nishati Jadidifu (Renewable Energy) ili kushajiisha uwekezaji wa umeme nchini, pamoja na kuwa na nishati ya kutosheleza kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda nchini. Utekelezaji wa hatua hiyo umeanza rasmi Julai, 2023.

vi. **Kuongeza Kiwango cha Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka Mauzo Ghafi TZS 50 milioni hadi TZS 100 milioni kwa Mwaka**

49. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia pendekezo la Serikali ya kuongeza kiwango cha usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka Mauzo Ghafi TZS 50 milioni hadi TZS 100 milioni kwa Mwaka ili kutoa fursa kwa walipakodi wadogo kujiimarisha sambamba na hatua ya Serikali ya kuwawezesha pamoja na kurahisisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwa walipakodi wadogo na wa kati. Hadi kufikia Machi, 2024 Jumla ya Walipakodi 396 wamesajiliwa na kuingizwa katika mfumo wa VAT. Utekelezaji wa hatua hiyo umeanza rasmi Julai 2023.

### E.2 Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali Nam. 11 ya Mwaka 2008

i. **Kupunguza Kiwango cha Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL) kutoka asilimia tano (5) hadi nne (4) na Kuongeza Idadi ya Waajiriwa Kutoka Waajiriwa wanne (4) hadi watano (5)**

50. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho ili kupunguza gharama kwa Mwajiri pamoja na kuongeza ulipaji wa

kodi kwa hiari kwa walipakodi. Utekelezaji wa hatua hiyo umeanza rasmi Julai, 2023.

### E.3 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015

#### i. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini

51. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuanza kutoza kiwango cha asilimia moja (1%) ya Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa ili kuongeza ufanisi wa miundombinu nchini. Aidha, hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 3.13 bilioni zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

#### j. Kutoa unafuu wa Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini

52. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia pendekezo la Serikali la kutoa unafuu wa Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa Nchini kwa Taasisi za Serikali ambazo zinahudumiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina, Miradi ya Washirika wa Maendeleo (Donor Funded Project), Wazalishaji waliosajiliwa (Registered Manufacturer) kwa uingizaji wa malighafi, pembejeo za viwandani na vifungashio, Umoja wa Mataifa na Taasisi zake na Ofisi za Ubalozi. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2023.

#### k. Kurudisha Kiwango cha Awali cha TZS 100 ya Kodi ya Miundombinu kwa Lita ya Mafuta ya Dizeli na Petroli.

53. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia pendekezo la Serikali kurudisha kiwango cha awali cha TZS 100 kwa lita ya mafuta ya Dizeli na Petroli kutoka **TZS 50** ili kuendelea kutoa fidia katika bidhaa hiyo, iwapo gharama za ununuzi zitapanda katika soko la Dunia au kupanda kwa gharama za usafirishaji. Aidha, Jumla ya **TZS 2.2 bilioni** zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

### I. Marekebisho ya Viwango Vya Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaolala Katika Hoteli za Zanzibar.

54. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuanza kutoza viwango vipya vya Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaolala Katika Hoteli za Zanzibar kulingana na Hadhi za Hoteli husika ili kuendana na mabadiliko makubwa ya Uchumi wa Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya **TZS 18.9 bilioni** zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

### E.4 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa No. 8 ya mwaka 2017

**Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa "Electronic Cigarettes" na "Shisha"**

55. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia pendekezo la Serikali la kutoza kiwango cha asilimia thelathini (30%) cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa "Electronic Cigarettes" na "Shisha" ili kupunguza matumizi ya bidhaa hizo kwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

### E.5 Marekebisho katika Sheria ya Tozo la Petroli Nam.7 ya Mwaka 2001

56. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kurudisha viwango vya awali vya Tozo la Petroli (TZS 350), Tozo la Kuendeleza Barabara (TZS 100) na Ada ya Usajili wa Njia (TZS 38) kutoka Tozo la Petroli (TZS 300), Tozo la Kuendeleza Barabara (TZS 70) na Ada ya Usajili wa Njia (TZS 15) kwa kuzijumuisha pamoja (mutawalia) kwa uingizaji wa mafuta ya Dizeli na Petroli. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya TZS 8.9 bilioni zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

### E.6 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya Mwaka 2017 Kuongeza Kiwango cha Presumptive Tax Scheme kutoka Mauzo Ghafi ya TZS 5 Milioni hadi TZS 100 Milioni

57. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia pendekezo la Serikali la kuongeza Kiwango cha "Presumptive Tax Scheme" kutoka Mauzo Ghafi ya TZS 5 Milioni hadi TZS 100 Milioni. Aidha, hatua hiyo imeondoa malalamiko kwa Wafanyabiashara wadogo ambao walikuwa wanalipa kodi ya mapato TRA na Ushuru wa Stempu ZRA. Kwa sasa Wafanyabiashara hao wanalipia kodi "Turnover Tax" ZRA pekee. Hadi kufikia Machi, 2024 Jumla ya Walipakodi 8,141 wameingizwa katika wigo wa kodi hiyo, na Jumla ya **TZS 8 Bilioni** zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

### E.7 Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi Nam. 7 ya Mwaka 2009

#### i Kufuta Adhabu (Penalty) kwa Walipakodi ambao wameshindwa kulipa kodi kwa wakati

58. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kufuta adhabu (Penalty) kwa walipakodi walioshindwa kulipa kodi kwa wakati, ambapo awali walitakiwa kulipa Adhabu (Penalty) na Riba (Interest). Aidha, hatua hiyo inakwenda sambamba na mifumo ya kodi kwa nchi zilizoendelea, pamoja na kuongeza ulipaji wa kodi kwa hiari. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya walipakodi 1,926 wamenufaika na utaratibu huu.

## F. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023-MACHI 2024.

59. **Mheshimiwa Spika,** Wakati nilipokuwa nawasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2023/2024; Serikali iliainisha Vipaumbele vya Bajeti tulivyopanga kuvitekeleza, na leo hii nina furaha ya kusema tumefanikiwa kutekeleza kwa zaidi ya asilimia 90 maeneo

tuliyoyawasilisha na kutekeleza maeneo mengine ya vipaumbele ambayo yalijitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti. Nathubutu kusema tumekamilisha na ziada ya matarajio yetu. Kwa uchache nitumie fursa hii kueleza miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kama ifuatavyo;

### a) Sekta ya Mawasiliano

60. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano kwa kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanaongezeka kwa watu wote hapa Zanzibar. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kufikisha mkonga wa Taifa wa Mawasiliano katika kila Wilaya na kufikia zaidi ya asilimia 95 ya vituo mbali mbali vya taasisi na kupelekea uhalisia wa upatikanaji wa Huduma ya Mawasiliano kufikia asilimia 100 katika maeneo yote yenye makaazi ya watu.

- **Sekta ya Usafirishaji wa Majini na Angani**

61. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu ya bandari, Serikali ilipanga kutekeleza mradi wa kuimarisha Bandari ya Mkoani ili kuiwezesha bandari hiyo kuendelea kuhudumia abiria na mizigo pamoja na kuteremsha makontena. Kiasi cha **TZS 6.77 bilioni** zimetumika kwa shughuli za kujenga sehemu ya kuhifadhi makontena, kuweka njia ya kupitia abiria, kujenga ukuta wa kuzuia mmong'onyoko wa udongo na kukarabati gati (Jetty) kwa kuziba nyufa na kurekebisha zege iliyo haribika.

62. **Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ni Ujenzi wa bandari ya Fumba yenye uwezo wa kuchukua makontena 3000 pamoja na sehemu ya kulazia lango la meli, kiasi cha **TZS 17.108 bilioni** zimetumika katika mradi huu ambapo **TZS 15.3 bilioni** zimejumuisha ujenzi wa bandari kutoka kwa muwekezaji na **TZS 1.808 bilioni** zimetolewa na Serikali kwa ajili ya gharama ya uwekaji wa miundo mbinu ya barabara na umeme.

63. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na kazi ya Ujenzi wa Jengo la Abiria la Pili katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA na kukamilika kwa Mpango wa Kulipa Fidia ili kuanza Ujenzi wa Jengo la Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

- **Kuendelea Kuimarisha Miundombinu ya Barabara**

64. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilihusisha Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu, Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini na Programu ya Ujenzi wa Barabara za ndani na vijijini ambazo zilipangiwa kutumia kiasi cha TZS 373.54 bilioni. Hadi Machi 2024, kiasi cha TZS 332.61 bilioni sawa na asilimia 89 zimetumika kwa ajili ya kufanikisha shughuli mbali mbali ikiwemo; usafishaji wa barabara, ujenzi wa madaraja, ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji kwenye kingo za barabara pamoja na njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano, ujenzi wa mabomba ya kupitishia miundombinu na uwekaji wa lami. Taarifa za kina juu ya utekelezaji wa miradi hii nimeziwasilisha katika Mpango wa Maendeleo niliowasilisha asubuhi ya leo.

**b) Kuimarisha Huduma za Jamii**

65. **Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili lilihusisha sekta mbali mbali za kijamii ikiwemo; sekta ya elimu, afya, usambazaji wa huduma za maji safi na salama sambamba na uimarishaji wa sekta ya michezo. Serikali ilapanga kutumia TZS 338.8 bilioni ili kufanikisha uimara wa utoaji wa huduma katika sekta hii, hadi kufikia Machi 2024, mafanikio ya sekta hizo ni kama ifuatavyo;

- **Sekta ya Afya**

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za afya bora kwa wananchi wote ili kupata taifa lenye siha na uwezo wa kuzalisha kwa maendeleo ya nchi. Serikali inaendelea kushirikiana na wadau mbali mbali katika kutoa huduma za afya kwa wananchi kwa kuzingatia sera na miongozo ya nchi. Hadi

kufikia Machi 2024, Serikali imefanikiwa katika maeneo yafuatayo;

i. Ongezeko la kiwango cha juu cha utoaji wa chanjo za watoto chini ya miaka mitano kutoka asilimia 85 hadi 95.
ii. Kuimarisha huduma za wagojwa mahututi kwa kuongezeka maeneo ya kutoa huduma hiyo kutoka eneo moja (1) hadi kufikia maeneo 14.
iii. Kuimarika kwa huduma za upasuaji kutoka vyumba vinne (4) (Theatres) hadi kufikia vyumba 34.
iv. Kupitisha Sheria ya Bohari Kuu ya Dawa kuwa Wakala sambamba na kuanza kazi kwa maabara mpya ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar.
v. Serikali imefanikiwa kujenga nyumba za makaazi ya Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya (Mwera pongwe, Kitogani na Pangatupu kwa Unguja na kwa upande wa Pemba Kinyasini na Vitongoji) na
vi. Kuanza kutoa huduma za matibabu kwenye hospitali mpya za Wilaya na Mkoa.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Sambamba na mafanikio haya, Serikali imerasimisha kada ya Wahudumu ya Afya ya Jamii wa kujitolea (Community Health Volunteers) na sasa kuwa wafanyakazi wa Afya Ngazi ya Jamii (Community Health Workers) na kuanzisha kitengo maalumu cha kusimamia shughuli za watoa huduma za afya wa ngazi ya jamii ili kuweza kudhibiti maradhi ya kuambukiza ikiwemo malaria, surua n.k.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ilianza utaratibu wa **Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF),** ambapo kila **Mtumishi katika Sekta ya Umma** alitakiwa kuchangia asilimia 3.5 kutoka katika mshahara wake na Serikali inachangia asilimia 3.5. Hadi kufikia Machi 2024, Mfuko wa Huduma za Afya ulikusanya **TZS 32.28 bilioni** sawa na asilimia 90 ya makadirio ya kukusanya **TZS 35.75 bilioni.** Fedha hizo zinajumuisha **TZS 30.5 bilioni** michango ya wanachama, **TZS 1.5 bilioni** fedha kutoka Serikalini, **TZS 2.5 milioni** ada ya maombi ya watoa huduma, **TZS 227.5 milioni** mapato yatokanayo na uwekezaji na **TZS 50 milioni** fedha kutoka

kwa Washirika wa Maendeleo kama msaada wa kitaalamu. Mfuko tayari umeshasajili wanachama 48,929 kutoka sekta ya umma na wanachama wategemezi waliosajiliwa wamefikia 18,764.

- **Sekta ya Elimu**

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kuimarisha miundombinu ya elimu yakiwemo majengo ya skuli, vyoo, maktaba pamoja na ununuzi na usambazaji wa samani, vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha **TZS 105.59 bilioni** zimetumika kwa ajili ya **Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu** sawa na asilimia 107 kwa ajili ya ujenzi wa skuli za ghorofa za msingi na sekondari.

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuwapatia wanafunzi mikopo ya elimu ya juu katika vyuo mbali mbali nchini. Hadi kufikia Machi 2024, idadi ya wanafunzi waliopatiwa mkopo wa elimu ya juu imeongezeka na kufika 6,137 ikilinganishwa na wanafunzi 4,875 mwaka 2022/2023 ambapo wanafunzi wapya 5,154 (wanawake 3,156 na wanaume 1,998) wamejiunga na vyuo vinne vya elimu ya juu.

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hichi, Serikali imeajiri wafanyakazi 679 katika sekta ya elimu, kati ya wafanyakazi 1,000 waliopangwa kuajiriwa kwa mwaka 2023/2024. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya wa umahiri kwa walimu 13,014 wa Maandalizi na Msingi wa Skuli za Serikali na Binafsi. Aidha Serikali imefanikiwa kukamilisha Rasimu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya elimu wa miaka saba 2023 - 2030 na mapitio ya Sera Mpya ya Elimu. Hatua iliyopo kwa sasa inaendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu ili kuenda sambamba na mageuzi hayo na malengo mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

- **Upatikanaji wa Huduma ya Maji Safi na Salama**

72. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inaendelea na jitihada za kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inaimarika katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Hadi Machi 2024, mahitaji ya maji kwa siku yamefikia lita 275,980,481 ambapo uzalishaji halisi umefikia lita 191,959,675 sawa na asilimia 70 ya uzalishaji ikilinganishwa na asilimia 67 ya uzalishaji iliyofikiwa Machi 2023. Juhudi zinaendelea kuchukuliwa kwa kutekeleza **Miradi ya Kimkakati** ili kuhakikisha huduma za maji safi na salama zinawafikia wananchi wote.

73. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na;
- Programu ya Miundombinu ya Maji, Hadi Machi 2024, jumla ya **TZS 2.6 bilioni** zimepatikana kwa ajili ya kununua vifaa vya maji, kujenga vibanda vya kuendeshea pampu, kununua mita za maji na kulipa fidia kwa wananchi walioathiriwa na ujenzi wa miundombinu ya maji katika maeneo ya Upenja, Chaani, Mchangani-shamba, Chumbuni, Makunduchi, Dunga Jumba la Mawe na Bungi.

- Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha TZS 25.16 bilioni zimepatikana (TZS 24.06 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 1.108 bilioni kutoka Serikalini), ambapo Uchimbaji wa visima 64 umekamilika pamoja na Ujenzi wa Matangi 15, Ulazaji wa mabomba kwa kilomita 453.7 na Ujenzi wa Ofisi. Aidha, malipo ya fidia yamefanyika kwa wananchi katika maeneo ya Mfenesini, Dole, Kizimbani na Kijichi pamoja na malipo ya Mshauri Elekezi.

- **Sekta ya Nishati ya Umeme**

74. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kupitia TANESCO na ZECO, katika kukabiliana na changamoto ya kuzidiwa kwa waya zetu zinazotumika kuingiza umeme Zanzibar kutoka Tanzania Bara, zipo katika hatua ya utekelezaji wa mradi wa kulaza waya mwengine wa baharini wenye uwezo wa Megawati 200 kupitia laini ya 220kV kwa Unguja na megawati 100 (100MW) kupitia laini ya 132kV kwa upande wa Pemba. Kukamilika kwa mradi kutapelekea kuwepo kwa umeme wa uhakika na wa kutosha.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeshasaini Mikataba kwa Kampuni ya Generation Capital Limited ambayo itazalisha Megawati 30 za umeme wa jua kwa Unguja katika eneo la Bambi na Kampuni ya ESR itakayozalisha Megawati 15 kwa upande wa Pemba. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa ZESTA ambao utazalisha Megawati 18 za nishati ya jua pamoja na mfumo wa uhifadhi wa umeme wenye uwezo wa Megawati 40 kwa saa moja. Sambamba na kutafuta kampuni zenye uwezo ambazo zitatakiwa kuzalisha Megawati 50 za gesi au nishati inayofanana nayo na Megawati 5 za umeme unaotokana na takataka. Hatua hii, itahakikisha upatikanaji wa vyanzo mbadala vya uzalishaji wa umeme wa uhakika unaoendana na uhifadhi wa mazingira yetu.

### c) Uimarishaji wa Ulinzi na Usalama

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ni nchi inayopokea wageni (watalii) kutoka katika mataifa mengi duniani ambapo Ulinzi na Usalama ni eneo la msingi ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika na kuweza kuchangia pato la taifa. Kwa mwaka 2023/2024 kiasi cha TZS 20.0 bilioni zimepangiwa kutekeleza shughuli za kuweka miundombinu mipya ya mawasiliano ya ulinzi na usalama; ununuzi wa vitendea kazi vya operesheni vya Idara Maalum za SMZ na kusimamia uendeshaji wa Mradi wa Mji Salama. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 13.057 bilioni sawa na asilimia 87 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya mradi huu.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kukuza na kuimarisha uzalishaji wa nguvu kazi ya taifa, Serikali imeendelea kuvitumia Vikosi vyetu vya Idara Maalumu za SMZ kushiriki katika Ujenzi wa Miradi mbali

mbali ya kimkakati. Naomba nitoe shukurani na pongezi kwa niaba ya Serikali, kwa ushiriki wao na kujitoa kwao bila kujali jua wala mvua. Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika naomba nitambue ushiriki wa kila kikosi katika Ujenzi wa Miradi ya Serikali;-

i. Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM): **Ujenzi wa Skuli,** Hospitali ya Vitongoji, Stendi ya Magari Darajani na Ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;
ii. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi: **Ujenzi wa soko la Kwanyanya Chuini;**
iii. Chuo cha Mafunzo: **Ujenzi wa soko la Jumbi;**
iv. Kikosi cha Valantia: Ujenzi wa **Ofisi za Masheha na Soko la Donge Mtambile;na**
v. Jeshi la Kujenga Uchumi: **Ujenzi wa Soko la Mwanakwerekwe, Mahkama ya Konde na Finya, Kituo cha Afya Kiuyu na jengo la Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba.**

**d) Kuimarisha Uchumi wa Buluu**

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uchumi Buluu ni kiunganishi cha mageuzi ya uchumi Zanzibar. Serikali imeendelea kuchukua jitihada kubwa ya kuweka mifumo ya kitaasisi ili kuifanya sekta hii kuendelea kuwa tegemeo katika kukuza uchumi wa wananchi na nchi kwa jumla. Miongoni mwa jitihada hizo ni kuwa na sera na sheria ambazo zitatumika katika utekelezaji na uendelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu ikiwemo **Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini.** Hadi kufikia Machi 2024, maeneo yaliyofanikiwa ni kama ifuatavyo;

i. Kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa samaki kutoka tani 61,794 zenye thamani ya TZS 391.37 bilioni hadi kufikia tani 80,085 zenye thamani ya TZS 569.07 bilioni kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 29.5;
ii. Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka tani 12,594 zenye thamani ya TZS 10.054 bilioni kwa mwaka 2022 hadi kufikia tani 16,653 zenye thamani ya TZS 16.514 bilioni kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 32.2;

iii. Kuzindua na kuanza kazi kwa Kituo cha Kijamii cha kutotolesha Vifaranga vya Majongoo Bahari Pujini, Pemba;

iv. Kutoa mafunzo ya teknolojia mpya ya kilimo cha mwani cha maji marefu kwa wakufunzi 95 (Unguja 31 na Pemba 64) wanaotarajiwa kufundisha kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi kwa mashirikiano na Shirika la IFAD;

v. Kuanzisha mashamba manne (4) ya majaribio ya mwani na majongoo bahari yaliyopo eneo la Chokocho, Wambaa na Muungoni;

vi. Utekelezaji wa ukondoishaji wa masuala ya Mpango Makhsusi wa Matumizi ya Bahari (Marine Spatial Planning); na

vii. Kuwasili kwa mtambo wa kuzalisha vinoo vya barafu wenye uwezo wa kutoa tani tano (5) sawa na vinoo sabini na mbili (72) zenye kilo 18 kutoka Kampuni ya Albacora ya Hispania ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Uvuvi wa kampuni hiyo na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Mtambo huu sasa unafanya kazi na upo katika Diko na Soko la Samaki Malindi.

**79. Mheshimiwa Spika,** Katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Udhibiti wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA), Serikali imefanya malipo ya fidia ya TZS 1.2 bilioni kwa wananchi walioathiriwa mali zao wakati wa zoezi la mtetemo, ambapo wananchi 3,575 walilipwa kati ya wananchi 4,330 waliothibitishwa kulipwa.

### e) Sekta ya Uwekezaji

**80. Mhehimiwa Spika,** kufuatia na kuanza utekelezaji wa **Sheria ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji ya Mwaka 2023,** kumetoa fursa nyingi kwa wawekezaji na kuimarisha huduma jumuishi kwa kuweka mfumo wa kielektroniki unaorahisisha utoaji wa huduma, kuweka ardhi ya akiba kwa uwekezaji, kuimarisha miundo mbinu ya uwekezaji katika **Maeneo Huru ya Uwekezaji ikiwemo Fumba, Micheweni na Dunga.** Hadi kufikia Machi 2024, TZS 9.69 bilioni zimetumika kwa kukamilisha **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji.** Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa

barabara km 13.5 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa ukuta katika **Maeneo Huru ya Uwekezaji Micheweni** ambayo yatakua ni kivutio cha uwekezaji, kukuza biashara na kuongezeka shughuli za biashara, usafirishaji wa bidhaa, ajira, pamoja na kuitangaza nchi kwa mataifa mbali mbali.

**81.** **Mhehimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2024; Serikali kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA); imefanikiwa kukuza Mtaji wa Uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani 1.499 bilioni kwa kusajili miradi 63 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 714.7 milioni. Miradi hiyo ya uwekezaji inatarajia kutoa ajira zipatazo 4,392.

### f) Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa maeneo ambayo Serikali imeyapa kipaumbele ni pamoja na kuinua uchumi wa Zanzibar na watu wake. Kutokana na juhudi zinazoendelea za kuwezesha wananchi kiuchumi, ikiwemo kutoa mikopo kwa wananchi wenye kipato cha chini katika sekta rasmi na zisizo rasmi, Serikali imefanikiwa kutoa mikopo ya vifaa vya ufugaji wa nyuki vyenye thamani ya TZS 29.96 milioni kwa vikundi ishirini na tano (25) ambavyo wamepatiwa mafunzo na kukaguliwa.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uwezeshaji ina lengo la kuinua kipato cha mwananchi na mjasiriamali kwa kuwawezesha kupitia mafunzo, mikopo na kuwaunganisha na masoko. Katika kukuza mitaji ya wajasiriamali Serikali imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya TZS 7.9 bilioni kwa wanufaika 2,045 (Unguja 1224 na 821 Pemba). Aidha, wajasiriamali wameunganishwa na masoko mbali mbali ya ndani na nje ya Zanzibar kupitia maonesho ya Afrika Mashariki, Sabasaba, Maonesho ya Mapinduzi, Maonesho ya fahari ya Zanzibar na Maonesho ya Marashi ya Karafuu, ambapo idadi ya Wajasiriamali waliounganishwa na masoko imeongezeka kwa asilimia 31 kutoka wajasiriamali 148 mwaka 2022/2023 hadi kufikia wajasiriamali 194 mwaka 2023/2024.

84. **Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, mafunzo ya Masoko ya Kidijitali yametolewa kwa watendaji 23 Unguja na Pemba watendaji 25. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wakufunzi hao kuweza kutoa mafunzo kwa wajasiriamali, kuhusu masoko ya kidijitali na fursa mbali mbali zinazopatikana katika mtandao ili kukuza masoko ya bidhaa zao na kukuza biashara zao na kuweza kujiinua kiuchumi.

85. **Mheshimiwa Spika,** Katika kukuza vipato vya wananchi kwa kuongeza mitaji yao kupitia Programu ya Urasimishaji wa Ardhi na Biashara, kiasi cha Hati za matumizi ya Ardhi 680 zimetolewa kwa wananchi ambazo zitatumika kama dhamana katika Taasisi za Kifedha na Mabenki kwa ajili ya kupata mikopo ambayo itasaidia kuimarisha hali zao na wategemezi wao ikiwa pia ni hatua ya kuleta maendeleo endelevu. Aidha, wafanyabiashara wadogo wadogo 200 wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa biashara katika mfumo rasmi na namna ya kuimarisha mitaji ili kukuza biashara zao.

86. **Mheshimiwa Spika,** Mafunzo hayo yametolewa kwa Wilaya ya Chake Chake kwa majaribio ambapo, wafanyabiashara 153 wamesajiliwa Biashara zao na kuingia katika mfumo rasmi unaowawezesha kufaidika na fursa za uwezeshaji zilizopo. Hatua za matayarisho za kutoa mafunzo kwa Wilaya zote za Zanzibar imekamilika. Utekelezaji wa Mradi huu unakwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 iliyoainisha kupitia Programu ya Urasimishaji wa Ardhi na Biashara kuwawezesha wananchi kiuchumi.

- **Ajira**

87. **Mhehimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, upatikanaji wa ajira rasmi za ndani umeongezeka kwa asilimia 65.9 kutokana na mikataba inayothibitishwa kutoka ajira 6,348 mwaka 2022/2023 hadi 9,630 mwaka 2023/2024. Ajira hizi ni kupitia Sekta ya Skuli Binafsi, Hoteli na Viwanda. Upatikanaji wa ajira nje ya nchi umekuwa kwa asilimia 285 kutoka ajira 1,080 mwaka 2022/2023 hadi kufikia ajira 3,078 mwaka 2023/2024. Ukuaji huu unatokana na sababu zifuatazo;

- Kuimarika kwa Sekta ya uwekezaji nchini,
- Kuwepo na mikakati imara ya kusimamia wakala binafsi wa ajira, na
- Kuimarika kwa Diplomasia ya nchi na mataifa mbali mbali ambapo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini mikataba ya mashirikiano na Nchi za Qatar, Saudi Arabia na Nchi za Falme za Kiarabu kwa lengo la kutoa fursa za ajira kwa vijana wa Kitanzania.

**g) Maendeleo ya Sekta ya Ardhi**

**88. Mheshimiwa Spika,** Serikali imesuluhisha migogoro ya ardhi 102 na kupatiwa ufumbuzi wake kupitia Kamati ya Usuluhishi wa Migogoro. Na kwa sasa Rasimu ya Miongozo ya Uthamini imeandaliwa ambayo itasaidia kupunguza changamoto katika masuala ya uthamini hasa wa fidia. Miongozo hiyo ni pamoja na Rasimu ya Muongozo wa Uthamini wa Fidia; Rasimu ya Muongozo wa Masafa ya Miti na Mazao (Trees and Crops Spacing); Rasimu ya Viwango vya Thamani za Ujenzi na Rasimu ya Muongozo wa Haki ya Matumizi ya Ardhi (Land Rates).

**89. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Serikali imefanikiwa maeneo yafuatayo;

i. Kupima viwanja 1,411 (843 Unguja na 568 Pemba) katika maeneo ya makaazi, taasisi, mashamba, eka na vitega uchumi pamoja na kupima vianzio vya upimaji 25 (15 Unguja na 10 Pemba);

ii. Kutayarisha ramani 2,351 (1,614 Unguja na 737 Pemba) na imekusanya taarifa 6 za Vipimo vya kupwa na kujaa kwa Maji ya Bahari. Vile vile, Serikali imefanikiwa kutayarisha ZUPIN 1,088 (632 Unguja na 456 Pemba) na kutoa taarifa za utunzaji na upatikanaji wa taarifa za Ardhi 1,469 (998 Unguja na 471 Pemba);

iii. Kutoa hati 880 (614 Unguja na 266 Pemba) za haki ya matumizi ya Ardhi, pamoja na kuhakiki Hati ya matumizi ya ardhi 367 (Unguja 247 na Pemba 120); na

iv. Kusajili Viwanja 552 (431 Unguja na 121 Pemba) na kutoa Mikataba ya ukodishaji wa ardhi kwa Wawekezaji 278 (257 Unguja na 21 Pemba).

- **Sekta ya Makaazi**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** Katika sekta hii, Serikali imefanikiwa kutenga maeneo 21 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu ikiwemo; Kitogani, Mwera Pongwe, Dunga, Matemwe Mbuyutende, Matemwe-Mlilile, Pale, Donge Kipange, Mkataleni, Kinduni, Mgambo na Matetema kwa Unguja na kwa upande wa Pemba maeneo hayo ni Finya, Konde, Tumbe, Sizini, Pujini, Gomisha-Wesha, Chokaani na Chokocho. Aidha, Serikali imefanikiwa kujenga nyumba 72 za makaazi eneo la Mombasa (Kwa Mchina) kupitia Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC) na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

- **Mazingira**

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kupunguza athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira Serikali imefanya ufuatiliaji wa maeneo 141 ya kimazingira kwa ajili ya kupunguza athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Maeneo hayo yanatokana na mashimo ya mchanga, kifusi, mawe na matofali ya mawe pamoja na yenye usimamizi duni wa taka na uchafuzi wa mazingira unatokana na viwanda vya matofali ya mawe.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza imekamilisha Ujenzi wa matuta yenye ukubwa wa mita cube 119m3 kwa ajili ya kuzuia mmong’onyoko wa udongo kwenye mabwawa pamoja na upandaji wa majani (vetiver) kwenye matuta na Ujenzi wa kituo kidogo cha kupima kina cha maji ya bahari (Tidal Measuring Station)

### h) Maendeleo ya Sekta ya Utalii

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi kwa kushiriki maonyesho ya utalii ya kimataifa ya ITB (Internationale Tourismus Börse) - Berlin, maonyesho ya wazi (Road Shows) katika nchi za Ujerumani (Cologne), Uholanzi (Amsterdam), Ubelgiji (Brussels) na Italy.

**94.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha utalii, katika upatikanaji wa taarifa za kutosha za watalii wanapoingia nchini. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania, Idara ya Uhamiaji, Ofisi za Taifa za Takwimu (NBS na OCGS) wanaendelea na utafiti wa utokaji wa wageni (Visitors Exit Survey) kwa mwaka 2023 ambapo, ripoti ya awali imeshawasilishwa katika ngazi ya Serikali. Utafiti huo utapelekea kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii, ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku pamoja na siku zao za ukaazi.

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mengine ni Pamoja na;-

i. Kuimarisha na Kuendeleza Maeneo ya Kihistoria, yakiwemo Ras Mkumbuu, Mangapwani, Maruhubi na Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni ambapo kiasi cha TZS 973.62 bilioni zimetumika;
ii. Kuandaa Mpango Mkuu wa Utalii wa Kisiwa Cha Pemba "Pemba Tourism Master Plan"; na
iii. Kuzindua Kampeni ya kijani na azimio la utalii Endelevu.

### i) Sekta ya Biashara na Viwanda

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali iliendelea kutafuta na kuimarisha Masoko na Usafirishaji wa bidhaa nje na kuangalia mwenendo wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar, sambamba na kuzitangaza bidhaa zinazozalishwa ndani ili ziweze kufikia ushindani wa kimasoko katika masoko ya Kanda yakiwemo ya Afrika Mashariki (EAC), Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Soko Huru la Afrika (AfCFTA).

**97. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2023/2024 mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa (GDP) umeongezeka kufikia asilimia 20 kutoka asilimia 19.4 katika mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa Sekta ya Viwanda hapa Zanzibar kupitia juhudi tofauti ikiwemo kukamilika kwa asilimia 80 ya ujenzi wa Eneo la Maonyesho ya Kibiashara Nyamanzi.

**98. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kufanya biashara ya mwani na hadi kufikia Machi 2024, Kampuni ya Mwani (ZASCO) imefanikiwa kununua wastani wa tani 724.8 za mwani aina ya Ulva. Mwani huo ulinunuliwa kwa gharama ya TZS milioni 779.8 na kuuza tani 575 kwa TZS milioni 786.6.

**99. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha **TZS 5.39 bilioni** zimetumika katika Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho ya Kimataifa Zanzibar na **TZS 8.36 bilioni** kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Parks) ambapo ujenzi wa barabara ya mzunguko katika eneo la mradi Dunga, umekamilika kwa kiwango cha lami; Mpango wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) katika eneo la Viwanda la Dunga umekamilika na ujenzi wa Mnara wa Tangi la Maji la lita 1,000,000 katika eneo la uwekezaji Dunga umefikia asilimia 32.4 na kwa upande wa Chamanangwe Pemba kazi inaendelea kwa kiwango kizuri.

### j) Sekta ya Fedha

**100. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekua ikifanya mageuzi kadhaa katika Sekta ya Fedha kwa kutambua umuhimu wa sekta hiyo katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini, ikiwa ni pamoja na kuandaa mfumo mzuri wa kifedha unaozingatia mahitaji ya huduma za kifedha. Mageuzi hayo yalilenga kuboresha sera za fedha, mifumo ya kisheria na udhibiti na kuimarisha huduma za kifedha (Soko la Mitaji na Dhamana, Benki, Hifadhi ya Jamii, Bima na Huduma ndogo za fedha) ambazo husaidia upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa muda mrefu.

- **Sekta Ndogo ya Benki**

101. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ndogo ya benki ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta inajumuisha Benki Kuu ya Tanzania ikiwa ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli za fedha nchini; benki za biashara; mawakala wa huduma za kibenki na mitandao ya simu. Kwa kipindi Julai 2023 – Machi 2024, sekta hii iliendelea kuimarika na hivyo kuchangia kwa wastani wa asilimia 2.3 katika ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar.

- **Amana**

102. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, amana katika benki zilizopo ziliongezeka hadi kufikia TZS 2,859.7 bilioni kutoka TZS 1,738.4 bilioni zilizokuwepo kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023. PBZ ilikuwa na asilimia 55.8 ya amana zote, ikifuatiwa na benki za NMB, NBC, CRDB na Amana Bank ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 30.2 ya amana zote.

- **Mikopo**

103. **Mheshimiwa Spika,** Mikopo ni sehemu ya rasilimali za benki ambapo kiasi kikubwa kinatokana na amana za wateja. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, thamani ya mikopo iliyotolewa ilifikia **TZS 2,393.35 bilioni,** ikiwemo Mikopo binafsi (ambayo zaidi inalenga wafanyakazi wa muda mrefu au wenye mikataba) ilichukua asilimia 37.9 ya mikopo yote iliyotolewa, sekta za kilimo, biashara na utalii ambazo kwa pamoja zilipata asilimia 29.6 na mikopo mengine ilielekezwa kwenye sekta ya utalii, mawasiliano ujenzi na nyenginezo.

- **Wakala wa Huduma za Kibenki**

104. **Mheshimiwa spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2024, idadi ya mawakala wa benki (agent banking) ilikuwa 2,376 ambao ni asilimia 2.8 ya mawakala wote nchini Tanzania. Pemba kulikwa na mawakala 418 na Unguja mawakala 1,958. Thamani ya miamala

pia iliongezeka maradufu kwenye kuweka na kutoa fedha. Kwa upande wa kuweka thamani ya miamala iliongezeka hadi kufikia TZS 1,872,798 milioni ukilinganisha na TZS 1,628,522.3 milioni 2022/2023 na kwa upande wa kutoa thamani ya miamala iliongezeka hadi kufikia TZS 699,780 milioni kutoka TZS 608,504.9 milioni mwaka 2022/2023.

- **Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni Nchini**

**105. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24, hadi kufikia Mei, 2024 shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,588.52 kwa dola ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,571.96 kwa dola ya Marekani kwa mwezi uliopita na shilingi 2,316.45 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23, ikiwa ni sawa na kupungua kwa thamani kwa asilimia 11.8 kwa shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani. Aidha, shilingi inaendelea kuimarika hali ambayo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, mfumko mdogo wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wa kibiashara, na nakisi ndogo ya urari wa bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje. Hali hii imechangiwa na hatua zilizochukuliwa katika kuongeza utulivu katika soko la fedha za kigeni nchini.

- **Huduma za Bima Zanzibar.**

**106. Mheshimiwa Spika,** Hali ya soko la Bima kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024 imeimarika. Biashara ya bima imekua kufikia asilimia 3 na kuwepo na ongezeko la watoa huduma ya bima kufikia kampuni kumi na saba (17) hapa Zanzibar, hivyo kuandikisha bima zenye thamani ya TZS 20.45 bilioni kwa mikataba ya bima 38,266 ambapo jumla ya TZS 5.8 bilioni zililipwa kama fidia kwa wahanga 3,364.

- **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar**

**107. Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Mfuko huu, ni kutoa hifadhi ya jamii kwa njia ya kulipa mafao kwa wanachama wachangiaji katika sekta za Serikali na Binafsi. Kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, Mfuko umesajili waajiri 237, waajiriwa 8,827 (wanachama kwa mfuko wa lazima) na Wanachama wa Mfuko wa Hiari 326. Hadi sasa Mfuko umekuwa na waajiri waliosajiliwa 3,029, waajiriwa waliosajiliwa 128,995 na Mfuko wa kujichangia kwa hiari waliosajiliwa 12,618.

**108. Mheshimiwa Spika,** Mapato ya uwekezaji kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, Mfuko umepata TZS 66.15 bilioni dhidi ya lengo la kupata TZS 64.09 bilioni sawa na asilimia 103, ukilinganisha na kipindi kama hiki mwaka uliopita ulipata TZS 46.19 bilioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 43.3.

**109. Mheshimiwa Spika,** Thamani ya uwekezaji kwa Mfuko, unajumuisha uwekezaji wa mabenki, hati fungani za Serikali na makampuni, hisa, uwekezaji wa majengo na mikopo. Hadi kufikia 31 Machi 2024, thamani ya uwekezaji wa Mfuko iliongezeka kwa asilimia 22.6 na kufikia TZS 958.8 bilioni ukilinganisha na uwekezaji kwa robo ya tatu ya 2022/23 kwa kiasi cha TZS 782.2 bilioni. Ongezeko hilo linachangiwa na uwekezaji wa ziada uliofanywa katika kipindi hicho kutokana na ongezeko la michango na mapato ya uwekezaji. Aidha, Kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, Mfuko ulipanga kuwekeza TZS 197.5 bilioni ambapo, gharama halisi za uwekezaji na usimamizi wa miradi zilikuwa TZS 180.95 bilioni sawa na asilimia 91.6 ya makadirio ukilinganisha na kipindi kama hiki Julai 2022-Machi 2023, Mfuko ulitumia TZS 159 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 14 ya uwekezaji.

**110. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mengine yaliyopatikana na Serikali kutokana na Mfuko huo ni pamoja na utekelezaji wa Miradi mbali mbali ya Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kiasi cha TZS 22.52 bilioni zimetumika kwa utekelezaji wa Miradi ifuatayo;-

i. Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya makaazi na biashara katika eneo la Viwanja Vya Magereza Unguja utakaokuwa na nyumba 276 za gharama nafuu na maduka ya biashara 42, hadi kufikia Mei 2024 kiasi cha TZS 9.017 bilioni zimeshatumika;
ii. Ujenzi wa kituo cha mabasi Kijangwani ambapo kiasi cha TZS 3.69 bilioni zimeshatumika hadi mwezi wa Mei 2024;
iii. Ujenzi wa kituo cha Michezo na Biashara Mbweni (Sports and Business facilities). Hadi kufikia Mei 2024 kiasi cha TZS 1.739 bilioni zimetumika;
iv. Ujenzi wa Kituo cha kisasa cha Mabasi na Maegesho Malindi kiasi cha TZS 3.56 bilioni zimetumika;
v. Ujenzi wa Soko la Mombasa kiasi cha TZS 3.94 bilioni zimetumika; na
vi. Ujenzi wa Kiwanja cha Mpira Matumbaku TZS 1,685.5 bilioni.

**111. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza na utekelezaji wa mafao mapya kama ilivyoelekezwa kwenye ilani ikiwemo Fao la kuumia kazini (Workers Compensation Benefit) na Fao la upotevu wa ajira (Unemployment Benefit), Mafao ambayo yameongeza imani kwa wanachama dhidi ya Serikali yao.

- **Taasisi zinazotoa Huduma Ndogo Ndogo za Kifedha**

**112. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa ni 1,645 (Unguja 791 na Pemba 854). Kati ya hivyo, SACCOS ni 3 na vyama vya uzalishaji na utoaji huduma ni 1,642. Vyama vya uzalishaji vinajumuisha kilimo mchanganyiko, huduma za maduka na biashara ndogo ndogo, ufugaji, uvuvi na kazi za mikono kama vile kupamba, uchoraji, uchongaji, kudarizi, fundi gereji nk. Zoezi hili limeongeza idadi ya vyama vilivyosajiliwa kufikia 5,713.

**113. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuviunganisha vyama vya ushirika 269 (Unguja 252 na Pemba 17) kwenye taasisi za fedha ambazo ni CRDB 165, PBZ 60, Azania 29 na Equity 15 na kuwawezesha kufungua Hesabu zao katika Benki hizo. Lengo ni

kurahisisha upatikanaji wa mikopo pamoja na kuwa na usalama wa kuhifadhi fedha za wanachama.

**114.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha zilizopata kibali kutoka Ofisi ya Rais fedha na Mipango ni (8) ambazo ni; ASA Microfinance Zanzibar Limited, TGT Microfinance Limited, Self Microfinance Fund Limited, Brac Zanzibar Finance Limited, Orbit Microfinance Limited, Platinum Credit Ltd-Tanzania, Vision Microcredit Limited na Taqwa Microfinance Limited. Aidha, Serikali pia katika hatua za kuimarisha usimamizi imezifungia Taasisi mbili (2) kutokana na kutoa huduma ndogo za fedha bila ya kuwa na kibali nazo ni; Fanikiwa Microfinance Company Limited iliyopo Unguja na Mtundi Microfinance Company Limited iliyoko Pemba.

- **Malipo ya Wahanga wa Ufilisi wa iliyokuwa Benki ya FBME**

**115.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Bima ya Amana na Wakala wa Ufilisi wa benki ya FBME nchini Cyprus walifanya tathmini ya fedha zilizopo mwezi wa Machi, 2024 na kupendekeza kwenye Kamati ya Serikali ya Majadiliano kuhusu ufilisi wa FBME Bank kulipa malipo ya awamu ya kwanza ya asilimia 30 kwa kila mdai.

**116.** **Mheshimiwa Spika,** Mnamo mwezi wa Aprili 2024, Bodi ya Bima ya Amana (DIB) iliunda Kamati ya Wadai wa FBME Bank kwa upande wa Tanzania iliyojumuisha wajumbe wawili (2) kutoka Zanzibar, wawili (2) kutoka Dar es Salaam, mjumbe mmoja (1) kutoka Arusha na mmoja (1) kutoka Mwanza. Aidha, tarehe 19 Aprili 2024, Kamati ilipata taarifa ya ufilisi wa benki ya FBME na kuridhia malipo ya awamu ya kwanza ya kiwango cha asilimia 30 kwa kila mdai aliyekuwa na amana zaidi ya kiwango cha fidia ya bima ya amana ya TZS 1,500,000 pamoja na kufanyika kwa malipo ya kundi la kwanza la wadai 500 ambao fomu zao za madai zilikuwa zimefanyiwa uhakiki.

117. **Mheshimiwa Spika,** Idadi ya wadai/wateja waliokuwa na zaidi ya shilingi 1,500,000 katika benki hiyo na kustahiki malipo ya ufilisi walikuwa 1,414 ambao wanadai Jumla ya TZS 35,231.7 Milioni. Kwa upande wa Zanzibar idadi ya wadai ni 757 na thamani ya madai ni TZS 20,823.9 Milioni, na Tanzania Bara idadi ya wadai ni 657 na thamani ya madai ni TZS 14,407.8 Milioni. Aidha, hadi kufikia tarehe 17 Mei 2024 Jumla ya wateja 452 kati ya 1,414 walikuwa wamelipwa fidia ya ufilisi ikiwa ni jumla ya TZS 3,325,690,340.92, Dola za Kimarekani 830,857.90, Paundi za Kiingereza 20,463.74 na Euro 7,943.87. Mchanganuo wa malipo haya ni kama ifuatavyo:-

i. Kwa upande wa Zanzibar idadi ya wateja waliolipwa ni 287 na walilipwa jumla ya Shilingi 1,755,488,552.97, Dola za Kimarekani 570,187.23, Paundi za Kiingereza 19,585.05 na Sarafu ya Euro 6,666.66; na
ii. Kwa upande wa Tanzania Bara idadi ya wateja waliolipwa ni 165 na walilipwa jumla ya Shilingi 1,570,201,787.95, Dola za Kimarekani 260,670.67, Paundi za Kiingereza 878.69 na Sarafu ya Euro 1,277.22.

- **Uendeshaji wa Mashirika ya umma**

118. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024, Serikali imefanya mageuzi ya usimamizi na uendeshaji wa Mashirika ya Umma, miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kutoa miongozo ya usimamizi wa Mashirika ulioleta tija ya utendaji na ukuzaji wa gawio kwa Serikali;
ii. Kutoa mikataba ya utendaji wa Bodi za Mashirika Zanzibar;
iii. Kufilisi kampuni ya ujenzi (kampuni ya JKU) ambayo ilikua haitengenezi faida;
iv. Kufanya ukaguzi wa utendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar na
v. Kusajili Mashirika mapya mawili (ZICTIA na ZHSF).

- **Fedha Kutoka Kwa Washirika wa Maendeleo Mikopo na Misaada**

**119. Mheshimiwa Spika,** Kufuatia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuridhia Mikutano ya Benki ya Dunia ya Tathmini wa Mzunguko wa 20 wa Muda wa Kati (IDA 20 MTR) kufanyika Zanzibar mwishoni mwa mwaka 2023, upatikanaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo unaendelea kuimarika kwa kasi kwa kuzidisha mahusiano mazuri yaliyopo kati ya Serikali na Washirika wetu wa Maendeleo. Kupitia Mikutano ile Zanzibar, iliweza kusikika Kimataifa, Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuongezeka kwa idadi ya wageni waliokuja kushiriki katika mikutano ya IDA 20 MTR ambapo takwimu zilionyesha kuwa wageni wapatao 300 walishiriki mikutano hiyo hapa Zanzibar. Wageni wengine, walirejea kutembelea Zanzibar baada ya mikutano ile.

ii. Kuongezeka kwa miradi mipya ishirini (20) ya maendeleo itakayopata fedha za Washirika wa Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inakadiria kupokea kiasi cha TZS 620 bilioni zitakazosaidia programu mbali mbali katika sekta za miundombinu, kilimo, afya, elimu, mahakama, maji na huduma nyenginezo. Kati ya fedha hizo, mikopo nafuu ni TZS 382 bilioni na misaada ni TZS 239 bilioni.

iii. Kuongezeka kwa kiwango cha Misaada ya Kibajeti (GBS) kutoka makadirio ya TZS 52 bilioni kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 hadi kufikia TZS 100 bilioni kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Fedha hizo zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

### k) Sekta ya Kilimo

**120. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024, imefanikiwa katika maeneo yafuatayo;

i. Kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju A, Kinyasini, Kibokwa, Kilombero Chaani

na Mlemele yenye jumla ya hekta 1,053. Miundo mbinu hii imeongeza tija katika uzalishaji wa mpunga na kufikia uzalishaji wa wastani wa tani 3-5 kwa hekta kwa msimu na tani 8-11 kwa hekta kwa mwaka,

ii. Uzalishaji wa miche 1,695,553 kati ya miche 2,000,000 iliyopangwa na kugaiwa kwa wakulima, ikijumuisha miche 804,053 imeoteshwa katika vitalu vya Serikali na miche 891,500 kwenye vitalu binafsi. Kati ya hiyo, 590,336 miche ya miti ya misitu, 134,777 miche ya mikarafuu, 49,050 miche ya minazi na 921,390 miche ya matunda na viungo,

iii. Kuongezeka kwa eneo la uzalishaji mpunga kufikia ekari 29,520 (Unguja 11,018 na Pemba 18,502) ambapo imepelekea ongezeko la mavuno kufikia tani 37,272 kutoka tani 27,947 na

iv. Kupandisha hadhi Msitu wa 'Kidikotundu-Nongwe-Vundwe' uliopo Mkoa wa Kusini Unguja, kutoka hifadhi ya jamii na kuwa Hifadhi ya msitu wa Serikali, hii itaongeza chachu ya utalii wa kimaumbile na Uhifadhi wa Bioanuai.

**121. Mheshimiwa Spika,** Mbali na mafanikio hayo katika sekta ya kilimo Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 1,064,58 bilioni na Dola za Kimarekani 43,419 kutokana na Ada ya kiingilio katika Hifadhi zetu za Jozani, Ngezi na Masingini ambapo watalii wapatao 55,870 (44,805 kutoka nje na 11,065 wa ndani) walitembelea katika hifadhi hizo.

### l) Utamaduni na Michezo

**122. Mheshimiwa Spika,** Katika kukuza na kuendeleza michezo, sanaa na utamaduni Serikali imepata mafanikio mengi kupitia mipango na mikakati ya utekelezaji wa programu mbali mbali ikiwemo;

- **Sekta ya Utamaduni**

**123. Mheshimiwa spika,** Katika kuendeleza utamaduni, Serikali iliwezesha kufanyika kwa Tamasha la 28 la Utamaduni wa Mzanzibari ambapo shughuli mbali mbali zenye mnasaba na tamasha hilo zilifanyika. Zaidi ya wajasiriamali 74 na vikundi 56 vya sanaa kutoka Unguja na Pemba vilishiriki. Maeneo mengine ni pamoja na;

i. Kuendeleza matamasha ya kijamii yakiwemo Tamasha la Mwaka Kogwa, ZIFF na Tamasha la Sauti za Busara.
ii. Kufanya mafunzo ya ufundishaji Kiswahili kwa Wageni kwa wahitimu wa Shahada ya Kwanza, walimu wa Sekondari na wadau mbali mbali wa lugha ya Kiswahili ambapo washiriki 101 wamehitimu mafunzo hayo.
iii. Kufanyika kwa Kongamano la Saba la Kiswahili la Kimataifa lililowajumuisha wadau na wanataaluma wa Kiswahili 258 kutoka ndani na nje ya nchi.

- **Sekta ya Michezo**

**124. Mheshimiwa Spika,** Katika kukuza na kuimarisha Michezo, Serikali imeziwezesha Timu za Taifa kushiriki katika mashindano ya CECAFA ya mpira wa miguu kwa vijana wenye umri chini ya miaka 15 (U-15) yaliyofanyika Uganda na chini ya miaka 20 (U-20) yaliyofanyika Kenya. Timu ya Vijana ya Zanzibar walio chini ya umri wa miaka 15 ilitwaa kombe la mashindano hayo. Hatua hiyo muhimu imeongeza hamasa kubwa kwa viongozi wa Serikali, wananchi, na wana michezo kwa ujumla. Mafanikio mengine katika sekta ya michezo ni pamoja na;

i Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo, kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za ujenzi wa viwanja vya wilaya na ukarabati wa viwanja vya michezo. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, kiasi cha TZS 31.709 bilioni sawa na asilimia 92.5 zimepatikana na kufanikisha Ukarabati wa viwanja viwili vikubwa, Kiwanja cha Amaan Complex Unguja na Kiwanja cha Gombani Pemba. Kwa sasa Serikali inaendelea

kukamilisha taratibu za kupata kampuni itakayosimamia na kuendesha Uwanja wa New Amaan Complex.

ii Michezo mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa imechezwa katika Viwanja vya hapa Zanzibar ikiwa pamoja na mechi za mpira wa miguu wa Kombe la Mapinduzi Zanzibar. Jumla ya timu 5 kutoka Zanzibar, 4 kutoka Tanzania Bara na timu 3 kutoka nje ya Tanzania zilishiriki katika mashindano hayo. Timu ya Mlandege kutoka Zanzibar ilifanikiwa kutwaa ubingwa wa mashindano hayo.

iii Michezo mengine ya kuogelea, Zanzibar ilishiriki mashindano ya para-olympic na kufanikiwa kupata medali 5 zikiwemo dhahabu na shaba.

iv Chama Cha Netball cha Zanzibar kimelipiwa ada ya mwaka ya uwanachama ili kuendelea kutambulika Kikanda na Kimataifa sambamba na kupatiwa mafunzo ya uongozi na mtaalamu kutoka Ujerumani kwa viongozi vijana 30 wanaoongoza michezo hapa Zanzibar.

**125. Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua kwa umuhimu wao Vijana wa Makachu Forodhani ambao wamekuwa wakileta hamasa sana katika mitandao ya kijamii na kuijengea Zanzibar umaarufu pamoja na kuvutia wageni mbali mbali.

**126. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inajivunia sana sekta ya michezo hususan katika ongezeko la wachezaji wanaotoka Zanzibar wanaochezea timu zilizopo Tanzania Bara ambao kwa kiasi kikubwa wanailetea sifa nzuri Zanzibar. Naomba kuchukua fursa hii kuwataja na kuthamini mchango wao kwa nchi yetu.

**127. Mheshimiwa Spika,** Nianze na Mchezaji Nambari moja mwenye jezi nambari 10 Mgongoni na Muamuzi mahiri wa timu ya Taifa ya Zanzibar Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi akifuatiwa na;

i. Feisal Salum Abdalla Fei Toto – Zanzibar Finest (Azam)
ii. Baraka Mtuli (Mashujaa FC)
iii. Shekhan Ibrahim (Yanga)
iv. Awesu Ali Awesu (KMC)
v. Ibrahim Abdallah Rashid BACA (Yanga)
vi. Seif Karihe (Mtibwa Sugar)
vii. Saleh Karabaka (Simba)
viii. Mudathir Yahya Abass – Zanzibar Greatest (Yanga)
ix. Abdallah Shaibu Ninja - Lubumbashi

- **Sekta ya Habari**

**128. Mheshimiwa Spika,** Serikali katika kuhakikisha inatoa miongozo katika sekta ya habari, imekamilisha Sera ya Habari ambayo itakuwa ndio dira ya kufuatwa katika utekelezaji na maendeleo ya sekta ya habari. Aidha, kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya UNESCO na Shirika la Habari la Internews iliandaa mafunzo maalum ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Maafisa Habari na Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye lengo la kuimarisha ujuzi wao katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano ndani ya Serikali. Katika maeneo mengine, Serikali imeweza;

i Kukarabati Jengo la Studio za Redio za Shirika la Utangazaji Zanzibar lililopo RahaLeo ili kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Mradi unatarajiwa kukamilika Julai 2024, na kugharimu kiasi cha TZS 9.56 bilioni.

ii Kuimarisha uunganishaji na usambazaji wa maudhui kwa kuidhamini Kampuni ya ZMUX mkopo wa TZS 4.5 bilioni ili kutekeleza Mpango wa Uwekezaji. Kupitia mpango huo, ZMUX itaboresha miundombinu ya kurushia matangazo, kufanya mageuzi ya kimfumo na ubora wa maudhui yatakayowezesha kuipa ushindani mzuri na kuipatia faida na kutoa gawio Serikalini.

iii Shirika la Magazeti limeweza kuchapisha na kuuza nakala zipatazo 942,000 za magazeti, nakala 7,000 za Jarida la "Neema Zetu" na kutoa matangazo 2,647 katika kipindi hichi.

iv Serikali imefanikiwa utoaji wa leseni 12 za vituo vya Utangazaji vinavyotoa taarifa mbali mbali kwa umma Unguja na Pemba kikiwemo kituo cha Televisheni cha DSTV, leseni saba (7) za maudhui ya mtandaoni na leseni nne (4) za vituo vya redio za FM.

v Serikali imesajili Waandishi wa Habari wapatao 173 hadi kufikia Machi, 2024.

- **Sekta ya Vijana**

**129. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza vijana na kuwapa nyenzo za uzalishaji mali, kiasi cha TZS 212.61 milioni na vifaa vya uzalishaji vyenye thamani ya shilingi 86.40 milioni vimetolewa kwa vikundi 330 na vijana mmoja mmoja 200 (117 Unguja na 83 Pemba) ili waweze kujiendeleza kiuchumi. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuwapatia mafunzo ya Ujasiriamali, Stadi za Maisha, Afya ya Uzazi, Elimu ya Uongozi na Uzalendo, mafunzo ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana, mafunzo ya amani na usalama, mabadiliko ya tabianchi na mafunzo ya TEHAMA kwa vijana 319,465.

ii. Kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 na kuzindua Sera mpya ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2023. Hatua hiyo muhimu inalenga kuimarisha mazingira bora ya Kisera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Kitaifa inayohusiana na ustawi na maendeleo ya vijana nchini.

iii. Kuanza na maandalizi ya "Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Vijana Zanzibar 2025-2030" ili kusaidia utekelezaji wa Sera na kutoa muongozo kwa wadau juu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya vijana.

iv. Kushiriki kwa vijana watano na kiongozi mmoja katika mkutano wa mtandao wa vijana wa Afrika 2023 uliofanyika nchini Kenya, Mafunzo ya Amani na Usalama yaliyofanyika nchini Uganda na Mkutano wa Usimamizi wa Mradi wa Vijana (SYP) uliofanyika nchini Botswana na

v. Vijana 1,979 wameweza kuhamasishwa na kushiriki katika shughuli mbali mbali za Kitaifa kwa lengo la kuwajenga moyo wa kuwa wazalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao.

### m) Uwajibikaji na Utawala Bora

**130.** **Mheshimiwa Spika**, Sote ni mashahidi kwa namna Serikali inavyochukua hatua stahiki kupambana na ubadhirifu na kuimarisha uwajibikaji kwa kuweka wazi taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuimarisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA).

**131.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia ZAECA, imefanya operesheni mbali mbali na udhibiti wa mianya ya rushwa na uhujumu uchumi. ZAECA pia ilifanya ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Miradi 96 ya Maendeleo Unguja na Pemba yenye thamani ya TZS 1.5 bilioni na Dola za Kimarekani 953 milioni. Kiasi cha TZS 9.09 bilioni zimeokolewa. Kati ya hizo TZS 8.4 bilioni zimerejeshwa Serikalini na TZS 676 milioni zimerejeshwa kwa wananchi kutokana na madai yao mbali mbali.

**132.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inaendelea kusimamia maadili ya viongozi wa umma ambapo kwa mwaka 2023/2024 imepokea na kuyafanyia kazi malalamiko manane (8) ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Serikali imeendelea kusimamia uwajibikaji kwa viongozi na watendaji wa sekta ya umma ambapo Fomu 2,685 za viongozi zimepokelewa na kusajiliwa. Viongozi wa Umma 250 wamehakikiwa sawa na 125% ya lengo la Viongozi 200 waliopangwa kuhakikiwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**133.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Serikali inaendelea kuimarisha ukaguzi wa ndani, ambapo hatua kadhaa za Sheria ya Ukaguzi wa Ndani zinaendelea, zikiwemo:-

- **Kuimarika kwa mazingira ya watumishi wa umma**

**134. Mheshimiwa Spika,** Katika kuongeza ufanisi na ari ya uwajibikaji kwa watumishi, Serikali imefanya marekebisho ya maslahi ya watumishi ili kuwawezesha kukimu ongezeko la gharama za maisha. Hadi kufikia Machi 2024 maeneo mengine yaliyofanikiwa ni pamoja na;

i. Kupatiwa mafunzo kwa watumishi wa umma wapatao 3,000 na kupelekea kuzidi makadirio yaliyowekwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya watumishi 2,700 kwa miaka 5.

ii. Kufanyika kwa tathmini ya Taasisi, ambapo Taasisi 15 zenye majukumu yenye kufanana, zimeunganishwa na Kampuni moja imefutwa. Lengo ni kupunguza wingi wa Taasisi, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za uendeshaji.

iii. Kubadilishwa kada kwa watumishi wenye sifa, kupandisha madaraja na kuthibitisha kazi ambapo idadi ya watumishi hao imeongezeka kutoka watumishi 220 hadi 952.

**n) Mashirikiano ya Kimataifa na kitaifa**

**135. Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jumuia ya Nchi za Afrika Mashariki, imekuwa na mahusiano makubwa ya kiuchumi na ya kidiplomasia kupitia ushiriki wa matamasha na makongamano ya ndani na nje ya Nchi, Mheshimiwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi amekuwa akishiriki katika masuala muhimu yakiwemo Siasa, Uchumi, Jamii, Diplomasia na Uwekezaji Miongoni mwa maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa yameleta mafanikio na athari kijamii na kiuchumi ni pamoja na;-

i. Kongamano la Kimataifa la Heart Team Africa lililofanyika Zanzibar;

ii. Jukwaa la 21 la Doha – Qatar viongozi, wawakilishi wa Serikali kutoka nchi mbali mbali Duniani walipata fursa kujadili masuala muhimu ya kimataifa, yakiwemo maendeleo, biashara, uchumi, mazingira, amani na usalama;

iii. Kusimamia hafla ya utoaji wa vyeti vya Uraia wa Tanzania kwa Tarjisi kwa wahamiaji wasiohamishika 3,319;

iv. Kupokea ugeni wa Rais wa Poland Mheshimiwa Andrzej Duda na Mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa nchini Tanzania na kupata fursa ya kujadili masuala muhimu yanayohusiana na vipaumbele vya maendeleo, ikiwa ni pamoja na uchumi wa buluu, elimu, afya, na miundombinu;

v. Kufanya mikutano na wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa pamoja na Makampuni Makubwa duniani ikiwemo UNICEF na UNESCO na kujadili juu ya utunzaji wa mji Mkongwe pamoja na kuboresha huduma za afya, elimu na usafi wa mazingira nchini na

vi. Mkutano wa majadiliano ya fursa za Uwekezaji kwa ujumbe wa Wafanyabiashara wa makampuni 20 ya Ufaransa uliofanyika Ukumbi wa ya Park Hyatty Zanzibar.

**136. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikifaidika na matunda ya uwepo wa wana Diaspora kutokana na kuendelea kuitikia wito wa Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi unaowahimiza kuchangia maendeleo katika nchi yao, Ujio wa ujumbe wa Madaktari Bingwa kutoka Taasisi ya Head Inc iliyopo Marekani ulifika Zanzibar na kuweka kambi ya Matibabu katika Hospitali ya Kitogani, Kusini Unguja. Taasisi hiyo ya Wanadiaspora wanaoishi nchini Marekani, ilitoa huduma ya matibabu ya ngozi, moyo, meno, macho, shinikizo la damu na kisukari kwa wananchi wapatao mia mbili (200). Sambamba na utoaji wa dawa, miwani pamoja na vifaa tiba vyenye thamani ya dola za kimarekani USD 225,000.

**137. Mheshimiwa Spika,** Maeneo mengine yaliyofanikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa programu ya kuratibu Wanadiaspora wataalamu kuja kubadilishana ujuzi na wataalamu wa Zanzibar (Transfer Of Knowledge Through Expatriate Nationals - TOKTEN) na imefanikiwa:

i Kuratibu ujio wa mtaalamu wa TEHAMA kutoka Kampuni ya biashara ya mtandaoni (Amazon) kutoka nchini Uingereza alietembelea na kutoa mafunzo katika Chuo Kikuu cha Taifa

cha Zanzibar (SUZA) na Jumuiya ya vijana ya "Pamoja Youth Initiative (PYI)".

ii Ujio wa Madaktari watatu wa Afya ya Akili kutoka Uingereza ambao walitembelea na kubadilishana ujuzi na Madaktari wa Hospitali ya wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu.

iii Utoaji wa misaada mbali mbali kwa wanajamii uliotolewa na Jumuiya ya Wanadiaspora wa Tanzania wanaoishi nchini Oman (TADIO) kwa kushirikiana na Taasisi za Al Wadood na Diaspora Charitable Group za nchini Oman katika Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba ikiwemo;

- Ugawaji wa sadaka ya futari kwa Wananchi 440 wa vijiji vya Tanga, Mkia wa ng'ombe, Limbani na Tungamaa,
- Ujenzi wa msikiti mkubwa katika kijiji cha Wingwi,
- Ujenzi na uzinduzi wa visima viwili katika kijiji cha Kinowe-Jiso.
- Kutembelea wazee, wajane na mayatima na kutoa msaada wa fedha,
- Ujenzi wa nyumba katika Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na
- Ufadhili wa masomo kwa wananchi wanaoishi kwenye mazingira magumu katika mikoa yote miwili ya Pemba.

## G. CHANGAMOTO UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI 2024

**138. Mheshimiwa Spika,** Mbali ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti, kumekuwa na changamoto mbali mbali ambazo zimeathiri ufanisi halisi wa bajeti hiyo katika baadhi ya mafungu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa gharama za ujenzi katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutokana na kubadilika mawanda (scope) ya miradi hiyo ukilinganisha na makisio ya awali yaliyoidhinishwa. Hii inapelekea kuhamisha fedha katika mafungu mengine kutekeleza miradi ya kimkakati na ambayo mawanda yake inabidi kubadilika kutokana na mahitaji.

ii. Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi kutokana na taratibu na matumizi sahihi ya mfumo wa manunuzi kunakosababishwa kwa kiasi kikubwa upungufu wa ueledi wa matumizi sahihi ya Mfumo wa Manunuzi.
iii. Changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni imeendelea kuathiri utekelezaji wa bajeti hususan katika malipo ya wakandarasi.

## H. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI 2023 HADI JUNI 2024

### a. Matarajio ya Mapato ya Julai 2023 - Juni 2024

139. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, hadi kufikia mwezi wa Juni 2024, Serikali inatarajia kukusanya TZS 2,946.44 bilioni sawa na asilimia 104 ya makadirio ya TZS 2,840.85 bilioni. Matarajio hayo yatafikiwa kutokana na mikakati ifuatayo ya kuimarisha mapato;

i. Kuendelea kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kuwafikia na kuwasajili walipakodi katika Mikoa;
ii. Kuendelea Kuimarisha Mifumo ya Uwasilishaji wa Ritani za Kodi na Utoaji wa Risiti;
iii. Kuunganisha Mfumo wa ZIDRAS na Mfumo wa Kodi za Ndani wa TRA, pamoja na Mfumo wa kufuatilia Wageni Wanaoingia Nchini (GADIF);
iv. Kufanya Mapitio ya Viwango vya Ada na Tozo zinazosimamiwa na Taasisi za Serikali; na
v. Kuongeza kasi ya ufuatiliaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha za Washirika wa Maendeleo na mashirikiano ya karibu na Wizara ya Fedha (SJMT) ili kuweza kuendelea kupata fursa zitolewazo na Washirika wa Maendeleo.

### 01. Mapato ya Ndani

140. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia **TZS 1,419.58 bilioni** sawa na asilimia 100 ya makadirio.

- **Mapato ya kodi**

141. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia **TZS 1,252.19 bilioni,** sawa na asilimia 102.9 ya bajeti ya **TZS 1,217.24 bilioni,** kwa mchanganuo ufuatao:
   i. Mamlaka ya Mapato Tanzania-Zanzibar (TRA) inatarajiwa kukusanya TZS 495.2 bilioni sawa na asilimia 95.1 ya mapato hayo;
   ii. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatarajiwa kukusanya TZS 735.98 bilioni sawa na asilimia 105.9 ya Makadirio, na
   iii. Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT inatarajiwa kufikia TZS 21 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

- **Mapato Yasiyokuwa ya Kodi**

142. **Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia **TZS 167.39 bilioni** sawa na asilimia 82 kwa mchanganuo ufuatao:-
   i. Mapato ya Wizara za Serikali yanategemewa kufikia TZS 140.39 bilioni ikiwa ni asilimia 91.6 ya makadirio ya mwaka ya TZS 153.28 bilioni;
   ii. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 22.5 bilioni ikiwa ni asilimia 64.3 ya makadirio ya mwaka ya TZS 35 bilioni na
   iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 4.5 bilioni ikiwa ni asilimia 33.3 ya makadirio ya mwaka ya TZS 13.5 bilioni. Upungufu huu ni kutokana na mabadiliko ya baadhi ya viashiria vya upatikanaji wa gawio hili.

**02. Mapato Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

143. **Mheshimiwa Spika,** Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia TZS 801.36 bilioni sawa na asilimia 117 ya makadirio ya TZS 686.61 bilioni, kwa mchanganuo ufuatao:-
   i. Misaada inatarajiwa kufikia TZS 151.12 bilioni, sawa na asilimia 144 ya makadirio ya TZS 104.94 bilioni;

ii. Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo unatarajiwa kufikia TZS 0.24 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya TZS 0.24 bilioni;
iii. Misaada ya Kibajeti (General Budget Support) inatarajiwa kufikia TZS 72 bilioni sawa na asilimia 138 ya makadirio na;
iv. Mikopo nafuu ya kisekta inatarajiwa kufikia TZS 592.01 bilioni, sawa na asilimia 112 ya makadirio ya TZS 529.24 bilioni.

### 03. Mapato Mengineyo

**144. Mheshimiwa Spika,** Matarajio ni kupokea TZS 710.00 bilioni ya Mapato Mengineyo sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 717.21 bilioni, kati ya mapato hayo;

i. TZS 150 bilioni kutoka mkopo wa Hati Fungani sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka mzima na
ii. Mkopo wa Serikali kwa miradi ya maendeleo unatarajiwa kufikia TZS 560.00 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya mwaka.

### 04. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

**145. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa matarajio ni kukusanya TZS 15.5 bilioni sawa na asilimia 86 ya makadirio. Hii inatokana na kupungua kwa ufanisi wa ukusanyaji kutokana na kutokuanza kwa uendeshaji wa masoko kuliko ilivyotarajiwa awali.

### b. Matarajio ya Matumizi ya Julai 2023 - Juni 2024

**146. Mheshimiwa Spika,** Kufikia Juni 2024, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 2,840.85 bilioni sawa na asilimia 100 ya bajeti ya mwaka ya TZS 2,840.85 bilioni ambapo;

i. Matumizi ya kazi za kawaida yanatarajiwa kufikia TZS 1,311.57 bilioni (zikiwemo TZS 9.2 bilioni za Mamlaka za Serikali za Mitaa) sawa na asilimia 99 ya makadirio;

ii. TZS 1,522.98 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo sawa na asilimia 101 ya makadirio ya awali (kati ya hizo TZS 608.42 bilioni ni kutokana na fedha za ndani, TZS 275.39 bilioni kwa ajili ya Mfuko wa Kugharamia Madeni; TZS 560 bilioni ni mikopo na TZS 79.17 ni misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na TZS 6.3 bilioni kwa matumizi ya maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**147. Mheshimiwa Spika,** ziada ya mapato inayotarajiwa kupatikana kutokana na makusanyo, itatumika kama bakaa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**148. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2024, Serikali inatarajia kukopa TZS 100 bilioni kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti, ambapo fedha hizo zinatarajiwa kukopwa kupitia, Hati Fungani za muda mrefu na Mikopo ya Ndani ya kibiashara.

## I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024

**149. Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2024 unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021-2026 (ZADEP); Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 na maelekezo na miongozo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati akilihutubia rasmi Baraza hili la kumi mwezi wa Novemba, 2020. Mpango huu umezingatia pia Sera na Mikakati ya Kisekta; Kikanda na Kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030.

**150. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.2 kutoka ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2023. Matarajio ya ukuaji huo utatokana na sababu zifuatazo:-

i. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 30 kutoka watalii 638,498 kwa mwaka 2023 hadi watalii 829,929 kwa mwaka 2024 kwa wageni wa kimataifa (international tourists) na kuongezeka kwa watalii wa ndani kwa asilimia 64.5 kutoka watalii 164,084 mwaka 2023 hadi kufikia watalii 270,000;
ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya Kimkakati ya maendeleo na miradi mengine ya ujenzi wa miundombinu itakayochangia ukuaji wa uchumi na huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama;
iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili ubaki katika tarakimu moja;
iv. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali;
v. Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;
vi. Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta za uchumi wa Buluu kama vile kuimarisha Matumizi Endelevu ya Bahari na kuwawezesha Wajasiriamali kwa kuwapatia elimu, uelewa na ufahamu zaidi, ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za ujasiriamali, uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini, mwani, biashara za baharini, utalii, mafuta na gesi asilia na nishati mbadala; na
vii. Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na jitihada za Serikali za kukuza uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira.

151. **Mheshimiwa Spika,** Misingi mikuu ya kukidhi ufikiaji wa matarajio hayo ni:

i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;
ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;

iii. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini na kwa nchi jirani; na
iv. Kuendelea kuimarika miundombinu na huduma za bandari zetu, ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu.

- **Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi jumuishi mwaka 2024/2025.**

**152. Mheshimiwa Spika,** Malengo na shabaha za uchumi jumuishi zilizozingatiwa katika Mpango wa mwaka 2024, ni kama ifuatavyo:-

i Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.2 mwaka 2024;
ii Mfumko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya kiwango cha asilimia 5 kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
iii Uwiano wa Mapato ya ndani kufikia asilimia 39.1 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 26 mwaka 2024;
iv Uwiano wa Mapato ya kodi kufikia asilimia 33 ya Pato la Taifa mwaka 2024 kutoka matarajio ya asilimia 22.4 mwaka 2023;
v Uwiano wa Deni na Pato la Taifa kufikia asilimia 15 mwaka 2024 kutoka asilimia 13 mwaka 2023;
vi Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2024;
vii Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kipindi kisichopungua miezi minne na nusu;
viii Kuendelea kutoa fursa kwa Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kupitia taratibu za Mashirikiano na Sekta ya Umma na Binafsi, utaratibu wa EPC+F na taratibu nyenginezo zilizopo; na
ix Matarajio ya upatikanaji wa ajira mbali mbali kufikia 21,808.

- **Uchumi wa Kidijitali (Digital economy)**

**153. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua hatua muhimu katika kutekeleza uchumi wa kidijitali kwa kutumia maendeleo ya kiteknolojia ili kuimarisha sekta mbali mbali. Uchumi wa kidijitali ni mwelekeo wa uchumi unaotegemea sana matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika shughuli za Kiuchumi, Katika uchumi wa kidijitali, biashara na shughuli za kiuchumi hutumia teknolojia ya kidijitali kwa njia mbali mbali, kama vile biashara mtandaoni, huduma za kifedha za kidijitali, uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa kutumia teknolojia, na mifumo ya kiotomatiki kwa usimamizi wa biashara.

- **Zanzibar na Uchumi wa kidijitali**

**154. Mheshimiwa Spika,** Serikali inalenga kuboresha miundombinu ya kidijitali, kama vile kupanua muunganisho wa intaneti na kuanzisha vituo vya teknolojia katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba kwa kushirikiana na makampuni ya mawasiliano ya simu kuimarisha Programu za kujenga uwezo na ujuzi wa kidijitali na kuwapatia wafanyakazi maarifa na ustadi wa kutumia zana za kidijitali na kutoa huduma kwa ufanisi. Huduma za Umma za kidijitali mtandaoni kama vile Serikali mtandao, huduma za kodi na leseni, habari na mawasiliano kwa umma ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi.

**155. Mheshimiwa Spika,** Jitihada hizi zinazochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na makampuni binafsi ya teknolojia na mashirika ya kimataifa zinalenga kukuza mfumo imara unaofaa kwa biashara ya kidijitali, ili kurahisisha huduma za umma, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, na kuiwezesha Zanzibar kuwa mdau mshindani katika uchumi wa kidijitali Duniani.

**156. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Sera ya ICT ya mwaka 2013 ya Zanzibar haina "policy statement" juu ya uchumi wa kidijitali, Hatua iliyopo sasa Serikali inafanya mapitio ya Sera hiyo kwa

lengo la kuainisha Uchumi wa Kidijitali ili iweze kutoa miongozo na kuweka sheria, na mikakati inayohusu uchumi wa kidijitali pamoja na kusimamia utekelezaji na Maendeleo yake. Hatua za msingi zitakazo chukuliwa na kuratibiwa ni pamoja na;

i. Kuwekeza katika Miundombinu ya TEHAMA;
ii. Kukuza Uwezo wa Kijamii na Kiutamaduni;
iii. Kuwezesha Mazingira ya Ubunifu na Uvumbuzi;
iv. Kukuza Elimu ya Kidijitali;
v. Kuweka Sera na Mipango ya Kisheria;
vi. Kuimarisha Usalama wa Kidijitali.

## J. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA UCHUMI NA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**157. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kuweka mfumo wa kodi uliotulivu na wenye kutabirika, kushajihisha ulipaji wa kodi kwa hiari, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika Sekta mbali mbali nchini. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**158. Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinazopendekezwa kuchukuliwa na Serikali ni kama zifuatavyo; -

a. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya Mwaka 1998

**Kuwajumuisha Watu Wenye Mahitaji Maalum**

i. Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Vifaa Vinavyotumiwa na Watu Wenye Mahitaji Maalum

**159. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji au usambazaji wa vifaa vinavyotumiwa na watu wenye mahitaji maalum ili kupunguza gharama za ununuzi wa

vifaa hivyo vikiwemo; Viti Mwendo (wheel chairs), viungo bandia (Artificial Limbs and Hands), visaidizi vya kuona na kusomea (programmable hearing aids), Fimbo Nyeupe (white canes) na Mashine za Kutolea Hati Nundu (Brailler Machine).

**Kushajihisha Uwekezaji katika Uchumi wa Buluu**

ii. Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Usambazaji wa Boti Zinazotengenezwa Nchini

**160. Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa usambazaji wa boti zimekuwa zikitozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hali hiyo imepelekea kuongeza gharama za uwekezaji katika Sekta ya uvuvi nchini. Hivyo, Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa usambazaji wa boti zinazotengenezwa nchini ambazo zitatumika katika shughuli za uvuvi na mwani nchini.

**iii. Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa Majokofu Makubwa na Gari Zenye Majokofu Nchini**

**161. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji wa Majokofu Makubwa au Gari zenye Majokofu kwa ajili ya kuhifadhia samaki ili kushajihisha uwekezaji katika Uchumi wa Buluu.

- **Kuimarisha Mchango wa Uchumi wa Kidijitali**

**iv. Kuoanisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika Huduma za Elektroniki (Digital Services)**

**162. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zimeanza kuwasajili na kuwaingiza katika mfumo wa Kodi ya Ongezeko la

Thamani (VAT), Kampuni zinazotoa huduma katika mitandao ya kijamii (online business platforms). Kampuni hizo tayari zimesajiliwa katika mfumo maalum wa kodi wenye uwezo wa kutambua muamala ulipofanyika katika pande zote za Muungano. Kwa sasa mfumo huo unatoza kiwango cha kodi cha asilimia kumi na nane (18%) wakati mfumo wa kodi wa VAT Zanzibar unatoza kiwango cha asimilia kumi na tano (15%). Hivyo, inapendekezwa kutoza kiwango cha asimilia kumi na nane (18%) ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Kampuni zinazotoa huduma katika mitandao ya kijamii ili kuondoa changamoto za utozaji wa kodi, pamoja na kulinda mapato ya Serikali. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza pato la Serikali kwa kiasi cha TZS 3.75 bilioni.

**v. Kuoanisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika Huduma za Bima**

**163. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la utoaji wa huduma za bima nchini, ambapo baadhi ya taasisi za fedha (Benki) na Mawasiliano (Mitandao ya Simu) zimekuwa zikitoa huduma hizo kama Wakala. Kwa kuwa mifumo ya kodi inatozwa katika kiwango cha asilimia 18, kumejitokeza changamoto ya mkanganyiko wa utozaji wa kodi hiyo baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Ili kuondosha changamoto hiyo, Serikali inapendekeza kuoanisha kiwango cha utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kuwa asilimia 18 kwa huduma za bima nchini badala ya asilimia 15 iliyopo sasa hivi. Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza mapato kwa TZS 3.57 bilioni.

- **Kuimarisha Uhifadhi wa Mazingira na Kushajihisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

**vi. Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa Mitungi ya Gesi ya Kupikia.**

**164. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25 inapendekezwa kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani

(VAT) kwa uingizaji wa Mitungi ya Gesi ya Kupikia ili kupunguza gharama za upatikanaji wake, kushajihisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, kuhifadhi mazingira pamoja na kupunguza matumizi ya mkaa.

**b. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

**i. Kutoa Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Gesi Nchini (Liquified Petroleum Gas - LPG).**

**165. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kwamba, Serikali inaongeza matumizi ya gesi kwa wananchi, pamoja na kupunguza madhara na athari za mabadiliko ya tabia nchi; inapendekezwa kutoa msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa uingizaji wa gesi nchini ili kushajihisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

- **Kuimarisha Uzalishaji wa Ndani Kuku na Samaki**

**ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kwa Uingizaji wa Kuku na Samaki Nchini**

**166. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko kubwa la uingizaji wa kuku na samaki wanaotoka nje ya nchi, hali ambayo imepelekea samaki na kuku wanaozalishwa nchini kukosa soko na hivyo kupoteza ajira kwa vijana na wananchi walio wengi. Vile vile, kumekuwa na kukosekana kwa soko kutokana na gharama kubwa za uzalishaji. Hivyo, Serikali inapendekeza kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Kiwango cha TZS 300 kwa kilo moja ya kuku (frozen chicken) au samaki (frozen fish) wakati wa uingizaji ili kushajiisha uwekezaji wa uzalishaji wa kuku na samaki, kwa lengo la kuongeza ajira, pamoja na kuwa na ushindani sawa katika soko la ndani.  Hatua hii inatarajiwa kuongeza pato la Serikali kwa TZS 3 bilioni.

**Kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Forodha**

**iii. Kuweka Utaratibu wa Uwekaji wa Stempu za Kielektroniki kwa Bidhaa Zinazoingia Nchini**

**167. Mheshimiwa Spika,** Nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania Bara zimeimarisha mifumo ya forodha kwa kuweka utaratibu wa Stempu za kielektroniki kwa bidhaa zinazoingia nchini ambazo hutozwa ushuru wa bidhaa. Hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 inapendekeza kuweka utaratibu wa uwekaji wa stempu za kielektroniki kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kutozwa ushuru wa bidhaa ili kuimarisha usimamizi, udhibiti pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hatua inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 0.5 bilioni.

**iv. Kuongeza Kiwango cha Kutozea Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Mvinyo na Vinywaji Vikali**

**168. Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kuongeza kiwango cha kutozea ushuru wa bidhaa za vinywaji vikali ikiwemo bia kama ifuatavyo:
Ushuru wa Bidhaa kwa Mvinyo itatoka TZS 2,466 hadi TZS 4,386 kwa lita moja.
Ushuru wa Bidhaa kwa Vinywaji Vyengine Vikali utapanda kutoka asilimia 35 hadi 70. Hatua hiyo itaongeza pato la Serikali kwa TZS 1 bilioni.

**v. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa "Sheesha" na Sigara za Kielektroniki yaani "Electronic Cigarettes"**

**169. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na wimbi kubwa la kuongezeka kwa matumizi ya "Sheesha" na Sigara za Kielektroniki "Electronic Cigarettes" hususan kwa vijana na watoto wadogo ambao ndio nguvu kazi ya Taifa. Hivyo, inapendekezwa Kuongeza kiwango cha kutoza Ushuru wa Bidhaa kutoka asilimia 35 hadi asilimia 120 ili

kuwalinda vijana, pamoja na watoto wetu ambao ndio nguvu kazi ya Taifa.

**c. Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

- **Kuimarisha Miundombinu ya Kijamii na Kiuchumi**

**i. Kutoza Kiwango Maalum cha Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaolala katika ya Visiwa au Vyumba vya Bahari**

**170. Mheshimiwa Spika,** Mfumo mzuri wa kodi unamtaka mlipakodi kulipa kodi kadiri kipato au matumizi yanavyoongezeka. Aidha, inaaminika kuwa, vyumba vya kulala vilivyoko katika visiwa au chini ya bahari gharama zake ni kubwa sana ikilinganishwa na vyumba vya kawaida. Hivyo, ili kuendana na mfumo bora wa kodi, inapendekezwa kutoza kiwango maalum cha Kodi ya Miundombinu cha Dola 10 za Marekani kwa siku kwa wageni wanaolala katika visiwa au vyumba vya chini ya bahari. Hatua hii inatarajiwa kuchangia TZS 3.5 bilioni.

**ii. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Kiwango cha Dola za Kimarekani**

**171. Mheshimiwa Spika,** Abiria wa kigeni wanaosafiri na vyombo vya baharini kwenda Tanzania Bara na ndani ya Zanzibar hukata tiketi kwa Dola za Kimarekani lakini kodi ya miundombinu hutozwa kwa Shilingi za Tanzania. Hali hii inakwenda kinyume na mfumo bora wa kodi kwani muamala wa ununuzi wa tiketi hufanywa kwa msingi wa Dola za Kimarekani wakati kodi hulipwa kwa msingi Shilingi za Tanzania. Hivyo, Ili kuondokana na changamoto hizo, inapendekezwa kutoza kiwango cha Dola za Marekani 2 badala ya TZS 2,000 kwa wageni wanaosafiri kwenda Tanzania Bara na kiwango cha Dola za Kimarekani cha Dola 1 badala ya TZS 1,000 kwa wageni wanaosafiri ndani ya Zanzibar. Hatua hii inatarajiwa kukusanya TZS 1 bilioni.

**d. Marekebisho ya Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari Namba 2 ya mwaka 1999**

- **Kuimarisha Miundombinu ya Bandari Nchini**

**i. Kutoza Ada ya Huduma za Bandari kwa Kiwango cha Dola za Kimarekani**

**172. Mheshimiwa Spika,** Abiria wa kigeni wanaosafiri na vyombo vya baharini kwenda Tanzania Bara na ndani ya Zanzibar hukata tiketi kwa Dola za Kimarekani ($) lakini ada ya huduma ya bandari hutozwa kwa Shilingi ya Tanzania. Hali hii inakwenda kinyume na mfumo bora wa kodi kwani muamala wa ununuzi wa tiketi hufanywa kwa msingi wa Dola za Kimarekani ($) wakati kodi hulipwa kwa msingi wa Shilingi ya Tanzania. Hivyo, ili kuondokana na changamoto hizo, inapendekezwa kutoza kiwango cha $ 2 badala ya TZS 2,000 kwa wageni wanaosafiri kwenda Tanzania Bara na kiwango cha $ 1 badala ya TZS 1,000 kwa wageni wanaosafiri ndani ya Zanzibar. Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 1 bilioni.

**ii. Kuongeza Kiwango cha Ada ya Huduma za Bandari kwa Abiria Wanaosafiri Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**173. Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa wageni wanaokuja Zanzibar na Meli za kitalii (Cruise Ship) au Meli ndogo za kitalii (Yacht) wanaposhuka na kutembea katika maeneo mbali mbali nchini wanatozwa kiwango cha Dola za Marekani 10 kama Ada ya Huduma za Bandari. Aidha, kiwango hicho kimepitwa na wakati na hakiendani na mabadiliko makubwa ya kiuchumi yanayoendelea na yanayohitajika hapa Zanzibar. Hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 inapendekezwa kuongeza kiwango hicho hadi kufikia Dola za Marekani 15. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali TZS 1.25 bilioni.

e. **Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Namba 7 ya Mwaka 2013**

- **Kuimarsisha Udhibiti na Usimamizi wa Gesi (LPG)**

i. **Kutoza Ada ya Udhibiti (Regulatory Levy) ya TZS 50 kwa Kilo kwa Uingizaji wa Gesi Asilia**

174. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji katika eneo ya Mangapwani, ambapo tayari Sekta Binafsi imeanza kuwekeza kwa kujenga Chelezo (Jetty) na Miundombinu ya Uhifadhi (Storage Facility) kwa ajili ya kushusha na kuhifadhi mafuta (Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa) na Gesi. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25 Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA) itaanza rasmi kuweka bei elekezeki kwa usambazaji wa gesi nchini kama ilivyo kwa mafuta. Hivyo, inapendekezwa kutoza TZS 50 kwa kilo moja ya gesi kama ada ya udhibiti (Regulatory Levy) wakati wa uingizaji bidhaa nchini. Hatua hii inatarajiwa kukusanya TZS 0.5 bilioni.

## K. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2024/2025

175. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) tunawajibu wa kutekeleza Mikakati ya Kimataifa na ya Kikanda. Kauli mbiu ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025 imebeba kauli mbiu ya "Kuendeleza Mageuzi ya Kiuchumi, Kupunguza Athari za Mabadiliko ya Tabianchi, na Kuimarisha Sera za Kibajeti kwa ajili ya Kuboresha Hali ya Maisha". yaani "Sustainable Economic Transformation through Fiscal Consolidation and Investment in Climate Change Mitigation and Adaptation for Improved Livelihoods" Katika kufanikisha hili Bajeti ya Serikali ya 2024/2025 itajikita katika kuendelea kuwekeza katika Miundombinu ya Uchumi, ikiwemo miundo mbinu ya barabara, kuimarisha uchumi wa wananchi, uhifadhi wa mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na ujumuishwaji wa watu wenye mahitaji maalum.

176. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Matumizi yanayowasilishwa katika Mwelekeo huu, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, yamezingatia uwezo wa mapato, kwa kuweka kipaumbele mahitaji ya matumizi ya lazima (statutory expenditure) kwa mpangilio ufuatao: mishahara, mahitaji ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali na vipaumbele vya taifa, maeneo mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na kugharamia miradi ya maendeleo inayoendelea na miradi yenye dhima kwa Washirika wa Maendeleo na miradi mipya ya kimkakati inayoendelea na inayotarajiwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na kugharamia utoaji wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya, elimu, maji na kuimarisha maeneo muhimu ambayo yatapelekea kukua kwa uchumi wa Zanzibar.

177. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mgao wa Bajeti katika mjumuisho wa Mapato na Matumizi (Aggregate Budget Revenue and Expenditure) umelenga kufanikisha shabaha na malengo ya Serikali katika maeneo yafuatayo:-

i. Maelekezo na Maagizo ya Serikali yanayotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ii. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025;
iii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2021-2026-ZADEP;
iv. Vipaumbele vya taifa na vya kisekta;
v. Mahitaji ya uendeshaji wa shughuli mtambuka; na
i. Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato.

178. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 yanakadiriwa kufikia **TZS 5,182.89 bilioni** ikiwa ni ongezeko la **TZS 2,342.05 bilioni** sawa na asilimia 54.81 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2023/2024 ya **TZS 2,840.85 bilioni.** Hii inaonesha ukuaji wa asilimia 82.44.

**179. Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu zilizopelekea kuongezeka kwa mapato hayo ni pamoja na:

i. Kuzijumuisha taasisi zinazojitegemea katika bajeti ya Serikali kwa kiasi cha TZS 202.61 bilioni awali hazikuwa zikijumuishwa katika Bajeti kuu ya Serikali;
ii. Kuongeza kiwango cha mkopo wa ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka TZS 717.21 bilioni hadi kufikia 1,712.00 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 138.7 kwa mwaka uliopita;
iii. Kuongezeka kwa utoaji wa fedha "Commitment" kwa Washirika wa Maendeleo kutoka TZS 686.61 bilioni hadi kufikia TZS 1,516.52 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 120.87 kutoka mwaka uliopita; na
iv. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kutokana na sera na hatua za kuimarisha mapato zilizopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**180. Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya makusanyo hayo yanajumuisha:

**a. Mapato ya Ndani**

**181. Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha TZS 1,732.83 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani sawa na asilimia 33.43 ya makadirio yote yanayotarajiwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Makadirio ya Ukusanyaji kwa Taasisi**

**182. Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Kodi yanakadiriwa kufikia TZS 1,467.06 bilioni yakiwemo:

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA kwa upande wa Zanzibar) TZS 600.08 bilioni;
ii. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) TZS 845.979 bilioni; na
iii. Mapato ya kodi yatokanayo na wafanyakazi kutoka SMT walioko Zanzibar TZS 21 bilioni.

**183. Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yamekadiriwa kufikia TZS 265.76 bilioni yanayojumuisha:-

i. TZS 217.26 bilioni, makusanyo ya Mapato ya Mawizara;
ii. TZS 35.00 bilioni, Gawio la Mashirika ya Serikali; na
iii. TZS 13.50 bilioni, Gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

**b. Mikopo ya Ndani**

**184. Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha TZS 1,712.00 bilioni sawa na asilimia 33.03 ya makadirio ya Bajeti yote zinatarajiwa kukopwa kupitia Benki na Taasisi za fedha za ndani ili kuziba Nakisi ya Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**c. Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**185. Mheshimiwa Spika,** TZS 1,516.52 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 29.26 ya makadirio ya bajeti yote ikiwemo:-

i. TZS 1,093.31 bilioni mikopo nafuu ya utekekelezaji wa Miradi ya Kisekta;
ii. TZS 322.95 bilioni misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
iii. TZS 260 milioni Mfuko wa Pamoja na Washirika wa Maendeleo "Buscket Fund" na
iv. TZS 100 bilioni ni Misaada ya Kibajeti.

**d. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**186. Mheshimiwa Spika**, TZS 18.94 bilioni Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na vyanzo vya tozo na ada, sawa na asilimia 0.37 ya bajeti yote.

**e. Mapato yatokanayo na Taasisi za Serikali zinazojitegemea**

**187. Mheshimiwa Spika,** TZS 202.61 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kutokana na mapato yatokanayo na Taasisi za Serikali zinazojitegemea sawa na asilimia 3.91 ya makadirio ya mapato yote.

### ii. Mapendekezo ya Mgao wa Matumizi

**188. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inatarajia kutumia TZS 5,182.89 bilioni zikiwemo:

### a. Matumizi ya Kazi za Kawaida,

**189. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 matumizi ya kazi za kawaida yanakadiriwa kufikia TZS 1,911.79 bilioni sawa na asilimia 36.89 ya makadirio ya bajeti yote ambayo yanajumuisha: -

i. TZS 893.60 bilioni Matumizi ya Mishahara;
ii. TZS 368.07 bilioni Matumizi ya Kuendeshea Ofisi;
iii. TZS 436.61 bilioni Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali;
iv. TZS 10.91 bilioni Matumizi ya Kazi za Kawaida ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mapato ya ndani na
v. TZS 202.61 bilioni Matumizi kwa Taasisi za Serikali zinazojitegemea.

### b. Matumizi ya Kazi za Maendeleo,

**190. Mheshimiwa Spika,** TZS 3,271.11 bilioni zimekadiriwa kutumika kwa Kazi za Maendeleo sawa na asilimia 63.11 ya bajeti yote zikiwemo:

i. TZS 1,862.00 bilioni kutoka Serikalini zinajumuisha TZS 640.25 bilioni Matumizi ya Miradi mipya ya kimkakati, TZS 312 bilioni kwa ajili ya mfuko wa kugharamia madeni (DSF) na TZS 909.76 bilioni miradi inayoendelea.
ii. TZS 1,401.07 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo TZS 1,093.31 bilioni Mkopo, na TZS 307.76 bilioni ni Misaada.

iii. TZS 8.03 bilioni Matumizi ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Miradi ya Mfuko wa Miundombinu**

**191. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Matumizi ya fedha za Mfuko wa Miundombinu kiasi cha TZS 76.439 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miradi maalum ya maendeleo kwa mwaka 2024/2025 ambapo, miradi ya Wizara nne imepangiwa kutumia fedha hizo ikiwemo;

i. Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe;
ii. Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki;
iii. Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu; na
iv. Ujenzi wa Skuli ya Meno.

## L. VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**192. Mheshimiwa Spika,** Kabla sijawasilisha vipaumbele vya bajeti naomba nichukue fursa hii, kwa waheshimiwa wajumbe wako wa Baraza hili tukufu na wananchi wote wa Visiwa vya Unguja na Pemba, kuifahamu dhana ya ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa Zanzibar. Tunapozungumzia ukuaji wa uchumi Zanzibar kwa lugha nyepesi haina maana kila mwananchi mfuko wake wa fedha utaongezeka, badala yake ni pale mwananchi anapoweza kuweka akiba kwa matumizi ya fedha kutokana na gharama ambazo angepaswa kutumia kwa ajili ya kupata huduma hiyo lakini badala yake Serikali inabeba gharama hizo kwa niaba yake. Mfano wa hili ni kama vile upatikanaji wa dawa hospitalini, chakula cha wagonjwa, ongezeko la mishahara ya walimu na madaktari na mengine mengi.

**193. Mheshimiwa Spika,** Sisi kama viongozi hatuna budi kusimamia misingi ya uadilifu na mikakati ya ukusanyaji wa mapato kwa kudai risiti kwa kila huduma tunayopatiwa. Hii itaongeza ari

na utayari wa wananchi na wao kulipa kodi. Kwa hili, naomba kuchukua fursa hii, kusisitiza na kutoa wito kwa wananchi wote, kuendelea kudai risiti na wafanyabiashara kutoa risiti kwa kila huduma zinazofanyika. Kwenye hili, tunapaswa kufahamu kuwa, huku tukielewa kwamba, kodi inayotozwa na wafanyabiashara inatokana na kodi tunazolipa sisi watumiaji wa huduma zao kupitia Kodi ya Ongezeko la Thamani na baadae Serikali huitumia kodi hiyo, kugharamia huduma za afya kwa baba zetu waliopo Kiwengwa na Mtambile, bibi zetu waliopo Rahaleo, Mkwajuni na Chasasa kule Wete, na mtoto wa Fatuma aliyeko Makunduchi na Pujini sambamba na kutoa huduma za elimu na maji kwa majirani zake walioko Pale na Likoni.

**194. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inaendelea kuchukua hatua kadhaa za kisera katika kuimarisha mapato na kusimamia matumizi ya Serikali zikiwemo;

i. Kuzijumuisha Taasisi zinazojitegemea katika Bajeti ya Serikali pamoja na kuhakikisha Taasisi hizo zinatoa mchango wa sehemu ya mapato yao katika Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali;
ii. Kuimarisha zaidi usimamizi wa kodi;
iii. Kuongeza wigo wa usimamizi wa miradi ya kimkakati kwa kuingia mikataba na Watoa Huduma Binafsi (outsourcing);
iv. Kuimarisha uwajibikaji wa Wakuu wa Taasisi zinazojitegemea, Mashirika na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zimepatiwa dhamana za mikopo kutoka Serikalini ili kuhakikisha kuwa, dhamana zinazotolewa zinalipwa kama ilivyokubalika. Wakuu wote wa Taasisi zinazopewa dhamana za Serikali, watawajibika kusaini Mikataba ili itumike kama kigezo cha ufanisi iwapo mikopo hiyo itakuwa inalipwa kama inavyopangwa;
v. Kuanza na Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2025 ikiwa ni pamoja na kuimarisha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;
vi. Maandalizi ya utekelezaji wa Bajeti Jumuishi zinazozingatia Jinsia na Usawa (Gender Responsive Budget and Equity) kwa Wizara sita za majaribio;

vii. Kuimarisha Umoja wa Kitaifa;
viii. Kuhifadhi na kusimamia mazingira ili kudumisha Usafi na kuweka Zanzibar katika hali ya kijani;
ix. Serikali kuzingatia ajira zenye mahitaji tu ili kupunguza gharama za mishahara. Sambamba na hilo, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya miundombinu ya kimfumo na ya kisera, ili Sekta Binafsi iweze kutoa ajira kwa vijana badala ya vijana hao kutegemea ajira ya Serikali pekee;
x. Kuendelea kuimarisha Maslahi ya Watumishi wa Umma ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi;
xi. Serikali itatoa kipaumbele cha pekee cha kutoa mikopo kwa wajasiriamali wa kutengeneza mashine za kuzalisha chakula cha kuku kwa lengo la kuwaimarisha na kuweza kuzalisha kwa wingi hapa nchini; na
xii. Katika kuimarisha uzalishaji wa ndani, Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali inakusudia kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda (Industrial Development Fund) ambao utaweka utaratibu wa kutoa vivutio kwa viwanda vitakavyowekeza Zanzibar.

**195.** **Mheshimiwa Spika,** Mkakati wa Serikali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo utazingatia zaidi utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayojikita zaidi katika kuimarisha hali za wananchi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali ili kuwezesha kuleta matokeo ya haraka katika kuhakikisha maendeleo ya nchi na wananchi yanapatikana kwa kutekeleza vipaumbele tulivyoviainisha.

**196.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Utaratibu Leo asubuhi nimewasilisha Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo. Kutokana na umuhimu wake naomba nisisitize machache katika maeneo niliyoyawasilisha ya vipaumbele. Kiasi cha TZS 2,087.71 bilioni zimetengwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025:-

### a. Kutumia Fursa za Uchumi Wa Buluu

**197. Mheshimiwa Spika,** Kama tujuavyo Sekta ya uchumi buluu ni moja katika sekta kiongozi katika uchumi wa Zanzibar, katika eneo hili Serikali imetenga kiasi cha TZS 453.039 bilioni sawa na asilimia 21.7 kwa ajili ya utekelezaji wa kipaumbele hichi ikiwemo:-

i. Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani TZS 257,53 bilioni (TZS 157.53 bilioni kutoka Serikalini na TZS 100 bilioni kutoka Africa Develoment Bank);
ii. TZS 15.00 bilioni zimekadiriwa kutumika katika Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria;
iii. Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki inakadiriwa kutumika TZS 27 bilioni;
iv. Ununuzi wa boti mbili za Serikali TZS 26.0 bilioni; na
v. Ujenzi wa Kituo cha Kivuko cha Abiria katika eneo la Maruhubi (Ferry Terminal at Maruhubi Area) TZS 127.5 bilioni.

### b. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

**198. Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili, Serikali imekadiria kutumia Jumla ya TZS 811.10 bilioni sawa na asilimia 38.8 katika programu mbali mbali zitakazo saidia kuongeza uzalishaji na kukuza ajira ikiwemo:

i. Programu ya ujenzi wa barabara kuu ambapo ujenzi huo unakadiriwa kutumia TZS 311.76 bilioni, (TSZ 115.53 bilioni kutoka Serikalini na TZS 196.23 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo);
ii. Programu ya Matengenezo ya Barabara za mjini TZS 112.09 bilioni;
iii. Programu ya ujenzi wa barabara za ndani TZS 45.6 bilioni;
iv. Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba TZS 101.39 bilioni (TZS 9.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 91.89 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo UKEF/CITY BANK);
v. Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati TZS 211.25 bilioni; (TZS 37.00 bilioni kutoka serikalini na TZS 174.25 Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - WB) na

vi. Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe TZS 29.00 bilioni.

**199. Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu wa kipekee, Serikali itafanya mazingatio maalumu ya ujenzi wa barabara za Uzi - Ng’ambwa, Kizimbani - Kiboje, Kitogani - Paje na kuzitengeneza upya barabara za Wete - Chake na Wete - Gando.

### c. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

**200. Mheshimiwa Spika,** Katika uimarishaji wa Mageuzi ya uchumi Zanzibar, Serikali imetenga kiasi cha TZS 65.32 bilioni sawa na asilimia 3.1 kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks) TZS 40.32 bilioni, na TZS 15 bilioni, na TZS 10 bilioni, kwa ajili ya kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar.

### d. Rasilimali Watu Na Huduma Za Kijamii

**201. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa tunatambua maendeleo ya nchi kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na Taifa lenye watu wenye Afya, Elimu na mazingira bora ya kuishi na kufanyia kazi katika eneo hili, Serikali imetenga kiasi cha TZS 674.627 bilioni sawa na asilimia 32.3 zikiwemo:-

i. TZS 417.52 kwa ajili ya Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu, (TSZ 234.389 bilioni kutoka Serikalini na TZS 183.13 bilioni ni Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo);
ii. TZS 35 bilioni Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi;
iii. TZS 6.47 bilioni Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika hospitali za Wilaya na Mikoa;
iv. TZS 21.00 bilioni kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja;
v. Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji safi na Salama Zanzibar, TZS 154.62 bilioni (TZS 43.50 bilioni

kutoka Serikalini na TZS 71.23 bilioni Msaada na TZS 39.88 bilioni ni Mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo); na

vi. TZS 40 bilioni Mradi wa Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo.

### e. Utawala Bora na Uhimivu

**202. Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili jumla ya TZS 83.62 bilioni sawa na asilimia 4 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Zanzibar Salama, Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa na Ujenzi wa Mji wa Serikali. Serikali pia itaendelea kuweka sera na mikakati ya kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi katika kujenga uchumi wa Zanzibar bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Aidha, pamoja na hayo, Serikali haitamvumilia mtu yoyote atakaehamasisha na kushiriki katika uvunjifu wa amani na utulivu uliopo, ubaguzi pamoja na kuhubiri mgawanyiko. Katika utekelezaji wa Bajeti hii, Serikali itazingatia mikakati ya kuimarisha umoja wa kitaifa ili mafanikio zaidi yaweze kupatikana.

- **Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025**

**203. Mheshimiwa Spika,** Utaratibu wa demokrasia kila baada ya miaka mitano hufanyika Uchaguzi Mkuu ambao unatoa fursa kwa kila mwananchi alietimiza sifa za kupiga kura kuchagua kiongozi ambae atasimamia Maendeleo ya Nchi, kupitia nafasi za Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wawakilishi wetu katika Baraza hili tukufu, Wabunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Madiwani wa kutuwakilisha katika Serikali za Mitaa.

**204. Mheshimiwa Spika,** Takriban tumebakisha mwaka mmoja na miezi michache kukamilisha kipindi cha kwanza cha awamu ya nane ya SMZ, kabla ya kufanya Uchaguzi Mkuu mwengine panapo majaaliwa, kwa bahati nzuri Nchi yetu kwa sasa iko katika Amani na Utulivu na wananchi sote katika Visiwa vya Unguja na Pemba tunaishi kwa mshikamano wa hali ya juu.  Nasaha zangu kwenu

vyama vya siasa na wafuasi wetu na wananchi wote kutanguliza mbele umoja wetu, Amani yetu na uvumilivu wetu kwa lengo la kuimarisha ustawi na uchumi wetu.

- **Malipo ya Madai ya tofauti ya Mishahara kwa Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

**205. Mheshimiwa Spika,** Mnamo Mwezi wa Aprili mwaka 2017 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa toleo la kuidhinisha mabadiliko ya mishahara kwa watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kufuatia toleo hilo taasisi zote zilibadilisha mishahara ya watumishi wao sambamba na viwango na vigezo vilivyoidhinishwa isipokuwa ZAWA walichelewa kuwafanyia marekebisho watumishi wake kwa kipindi cha miezi 15 tokea kutolewa kwa toleo hilo, hali iliyosababisha malalamiko ya watumishi hao juu ya haki zao stahiki. Napenda kutoa taarifa kuwa Serikali imeshakamilisha taratibu zote za kufanya malipo kwa malimbikizo ya Mshahara ya muda mrefu kwa wafanyakazi wa ZAWA; ambapo kiasi cha TZS 1.17 bilioni kitalipwa kwa jumla ya watumishi 642, kati yao walioko kazini ni 453. Waliostaafu 131, waliohamishwa kwenda Taasisi nyengine 26 na waliofariki 32 taratibu za kuwapata warithi wa marehemu tayari zinaratibiwa na Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar, malipo hayo yatafanyika ndani ya mwezi huu wa Juni, 2024 kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha.

- **Mageuzi ya Bajeti Inayozingatia Jinsia na Usawa**

**206. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025 Serikali inaendelea na mageuzi ya bajeti inayozingatia jinsia na usawa kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Mageuzi hayo yanaratibiwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Jitihada mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo kujenga uelewa kwa Taasisi zote za Serikali pamoja na Kamati ya bajeti na wenyeviti wakudumu wa Kamati zote za Baraza la Wawakilishi.

207. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imetenga kiasi cha TZS 59.48 bilioni kwa wizara sita za mfano ambapo wizara hizo bajeti zao zimehusisha moja kwa moja masuala ya kijinsia na usawa katika bajeti ya mwaka 2024/2025. Wizara zilizochaguliwa ni; Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili, na Mifugo na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

208. **Mheshimiwa Spika,** Wizara hizo kupitia Hotuba zao za mwaka 2024/2025 walizo ziwasilisha katika Baraza Hili wameainisha maeneo hayo pamoja na shabaha walizojiwekea. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wameandaa utaratibu maalumu na mikakati kwa kupimwa utekelezaji wa Shughuli zilizoainishwa zinazohusiana na GRB &E na kuzingatiwa wakati wa ufuatiliaji ili kuhakikisha malengo ya shughuli zilizoidhinishwa na shabaha zilizopangiwa zinafikiwa.

209. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa maeneo yaliyohusishwa na jinsia na usawa ni pamoja na masuala ya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake,wanaume na watoto katika kukabiliana na vitendo vya ukatili, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa wajasiriamali na fursa za mikopo, vifaa vya watu wenye mahitaji maalum ya vijana na wanafunzi, upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanawake katika mnyororo wa thamani wa Uvuvi na kilimo cha Mwani, Kupunguza idadi ya vifo vya mama wajawazito na watoto wakati wa kujifungua na Kuongeza Idadi ya Wanawake wanaopatiwa msaada ya kisheria na haki.

## M. UGHARAMIAJI WA NAKISI YA BAJETI.

210. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutekeleza sera za bajeti ambazo zitaiwezesha ukuaji wa mapato ya ndani kwa kuongeza jitihada za ukusanyaji wa kodi na tozo mbali mbali kupitia matumizi sahihi ya mifumo ya kieletroniki na ukuaji wa Uchumi kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati na sera za uwekezaji,

sambamba na kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu. Kwa mwaka 2024/2025, Serikali inatarajia kukopa Jumla ya TZS 1,712.00 bilioni ikiwa ni mikopo ya Hati fungani na mikopo ya Kibiashara kupitia taasisi za kifedha, benki za ndani na nje na mifuko ya hifadhi za jamii kwa ajili ya kuziba nakisi ya Bajeti, ili kugharamia shughuli za Serikali hususan utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

## N. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2024/2025

211. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kiwango cha utegemezi wa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kinakadiriwa kufikia asilimia 6.3 kulingana na matarajio ya kupokea TZS 322.95 bilioni ikiwa ni Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kiwango hicho bado ni himilivu na bado kimo katika mipaka iliyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 Kifungu Nambari 139 (iii).

## O. MAZINGATIO YA MAENEO MAHSUSI KWA BAJETI YA 2024/2025

212. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali itaendelea na uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa Miundo mbinu na huduma za Kijamii na Utekelezaji wa Sera za Kiuchumi. Mazingatio Mahsusi katika bajeti ya 2024/2025 yakiwemo;

i. Kuanza Malipo ya nauli kwa watumishi wote wa Serikali, ambapo kiasi cha TZS 34 bilioni zimetengwa kwa ajili ya malipo ya TZS 50,000 kwa kila mtumishi,

ii. Kuongezeka kwa posho la likizo kwa watumishi wote wa Taasisi za Umma, Serikali imetenga kiasi cha TZS 2.13 bilioni. Mazingatio maalumu pia yamewekwa wa watumishi na watendaji wa Baraza la Wawakilishi katika kuimarisha utendaji wao.

iii. Serikali imetenga kiasi cha TZS 47.53 bilioni kwa ajili ya ajira mpya zenye uhitaji.

iv. Kukamilisha maandalizi ya uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji

Zanzibar na Soko la Hisa la Zanzibar;

v. Kukamilisha Rasimu ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato Yatokanayo na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia; na

vi. Kuendelea na mageuzi ya taasisi za umma kwa kufanyika tathmini ya majukumu ya kitaasisi. Jumla ya taasisi 15 zenye majukumu yenye kufanana zimeunganishwa na Kampuni ya Ujenzi wa Taasisi za Serikali imefutwa kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

## P. SHUKURANI

**213. Mheshimiwa Spika,** Naomba nimalizie na hotuba yangu kwa kumpongeza tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa namna alivyoweza kuibadilisha Taswira ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia upangaji hadi utekelezaji wake na kuonesha kwa vitendo dhana na maana halisi ya Bajeti Inayozingatia Matokeo (PBB). Sote tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kumneemesha siha njema ili aweze kufikia azma na dhamira yake kwa ufanisi na mafanikio makubwa.

**214. Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nimpongeze Naibu Waziri, Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango Mheshimiwa Juma Makungu Juma kwa ushirikiano wake na kujitoa kwake kwa kuhakikisha sekta ya fedha inaimarika. Mashirikiano yake kwa pamoja yamewezesha Ofisi yetu kufikia malengo iliyojiwekea. Naomba kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Kijini kuwa, Mheshimiwa Juma Makungu Juma anafanya kazi njema na anajitoa katika kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar kupitia jukumu lake la Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango.

**213. Mheshimiwa Spika,** Kipekee nimpongeze, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, Dkt. Juma Malik Akil; Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh, Naibu Katibu

Mkuu Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango CPA Aboud Hassan Mwinyi, Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA Hamad Saleh Hamad, Mkaguzi Mkuu wa Ndani CPA Fatma Khamis Mohammed, pamoja na Watendaji Wakuu na watumishi wote wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa mashirikiano na mshikamano wao wa dhati hadi kukamilisha mchakato wa Bajeti ya Serikali. Bajeti hii isingekamilika bila ya mchango wa watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara na Idara za Serikali; nao wote kwa pamoja nawapa shukurani zangu za dhati. Kwenye hili, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kipekee inapongeza juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar pamoja na Wanasheria wote waliopo katika Ofisi yao kwa namna ambavyo wameendelea kusimamia misingi ya kisheria katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Aidha, tunaipongeza Taasisi ya Rais ya Ufuatiliaji (Presidential Delivery Bureau) kwa uweledi wanaouonesha katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais.

215. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kuwa dira ya kufikia malengo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa Zanzibar ya kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuwa tegemeo kubwa sana la wananchi na hivyo uimara wake ndio uimara wa Serikali na ustawi wa Maisha ya Wazanzibari wote. Serikali pia inaendelea kuvipongeza vyama vyengine vya siasa vikiwemo Chama Cha ACT-Wazalendo, Chama cha ADA-TADEA, Chama cha wananchi CUF kwa kuendelea kuweka na kuimarisha misingi ya kudumisha amani na utulivu hapa Zanzibar.

216. **Mheshimiwa Spika,** Natambua kuwa uongozi ni dhamana na dhamana ni deni. Sisi kama viongozi hatuna budi kubeba dhamana hii kwa uadilifu mkubwa ili kulipa deni hili kwa wananchi tunaowawakilisha. Tunatakiwa kuhakikisha wananchi wenzetu wanafurahia manufaa ya kuwa Wazanzibari, kwa kuhakikisha usimamizi wetu kwao unaakisi matarajio yao kwa Serikali inayowaongoza.

**217. Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa shukurani zangu ziende kwa Washirika wetu wa Maendeleo ya Ndani na Nje walio tuchangia bajeti hii inayoendelea na wanaotarajia kutusaidia katika Bajeti yetu ya Serikali kwa 2024/2025. Naomba niwataje kama ifuatavyo; United Nations Children's Fund (UNICEF), Global Environment Facility, Africa Development Bank (AfDB), Germany, International Fund for Agricultural Development (IFAD), NORWAY, Sweedish International Development Agency (SIDA), United Nation Population Fund (UNFPA), World Intellectual Property Organization (WIPO), World Bank (WB), Global Partnership for Education (GPE), United State Agency for International Development (USAID), European Union (EU), Saudi Fund (SF ), BADEA, Sweden, Costech, World Health Organization (WHO), EXIM Bank India, Khalifa Fund (KF) KOREA, KOICA, United Nation Environment Programme (UNEP), OMAN, JICA, IRISH EMBASSY, UKEF/CITY BANK, STBF, QUEEN'S Belfast University, AUSTRIA, KFWNORAD, UN AIDS, NERTHERLAND, EXIM Bank china, EXIM BANK (KOREA) and SPAIN pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**218. Mheshimiwa Spika,** Nazishukuru vile vile Asasi Zisizo za Kiserikali ambazo zimeendelea na utekelezaji wa miradi mbali mbali katika maeneo ya sekta za afya, elimu, kilimo, uwezeshaji wa wananchi, uwajibikaji na usimamizi wa sera za Serikali. Pongezi za kipekee tunaziwasilisha kwa Benki zetu za ndani zikiwemo PBZ, CRDB, NMB, NBC, TCB, Azania, Absa kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

**219. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ambayo tunayaona sasa yanatokana na misingi imara ya waasisi wetu. Ambao kwa namna moja ama nyengine, wameshiriki katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi chao. Bajeti tunayoisoma leo ni Bajeti inayotimiza miaka 60 tokea kuanzishwa kwa Wizara inayosimamia masuala ya fedha hapa Zanzibar mara baada ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Naomba kuwatambua wale wote. Wale waliokuwa wameshatangulia mbele ya haki, tunamuomba Allah awape makaazi mema peponi na wale ambao bado wapo hai,

tunamuomba Allah (S.W) awape afya na siha na waendelee kutoa mchango wao kwa Zanzibar popote pale walipo. Viongozi wenyewe ni kama wafuatao:Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilisimamiwa na :-

i. Marehemu Hasnuu Makame - (1964-1965)
ii. Marehemu Abulazizi Ali Khamis - (1966-1967)
iii. Marehemu Tawakal Khamis Tawakal - (1968-1978)
iv. Marehemu Ramadhan Hamad Hilika - (1978-1979)
v. Marehemu Makame Khamis Komba - (1979-1980)
vi. Marehenu Taimur Saleh Juma - (1980-1981 na 1984-1988)
vii. Marehemu Jaffar Mfaume Ali - (1988-1990)
viii. Balozi: Amina Salum Ali - (1990-2000)
ix. Marehemu Suleiman Othman Nyanga - (2000-2005)
x. Marehemu Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - (2005-2010)
xi. Balozi: Omar Yussuf Mzee - (2010-2015)
xii. Dkt. Khalid Salum Mohammed - (2016-2019)
xiii. Balozi: Mohammed Ramia Abdiwawa - (1981-1984 na 2019-2020)
xiv. Jamal Kassim Ali - (2020-2022).

**220. Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa Bajeti hii imesomwa hapa leo na Dkt. Saada Mkuya Salum ambae ni tunda na zao la Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni mwanamke wa pili kushika nafasi hii muhimu kwa maendeleo ya taifa akitanguliwa na Mheshimiwa Balozi Amina Salum Ali aliyeongoza Ofisi hii muhimu sana kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 1990 hadi 2000.

Tunawashukuru na kuwapongeza wote hao kwa misingi imara waliyoiweka ambayo inaendelea kuwa dira na nuru ya kufikia malengo tuliyojiwekea kama Serikali pamoja na nchi kwa ujumla. Kila mmoja kwa nafasi yake ameweza kutoa mchango wake mkubwa ambao umeleta mafanikio tunayoyaona leo. Michango yao hiyo, itaendelea kukumbukwa na kuthaminiwa kila iitwayo leo.

## Q. HITIMISHO

221. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Makadirio ya mapato ya Serikali ya kukusanya **TZS 5,182,89 bilioni** (Shilingi trilioni tano, bilioni mia moja themanini na mbili, milioni nane themanini na tisa). Kati ya mapato hayo, **TZS 4,961.343 bilioni** Makusanyo ya Serikali Kuu, yakiwemo; mapato ya ndani ni **TZS 1,732.83 bilioni,** Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **TZS 1,516.52 bilioni,** Mikopo ya ndani kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo ni **TZS 1,712.00 bilioni.** Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa **TZS 18.94 bilioni** na Taasisi za Serikali zinazojitegemea ni **TZS 202.61 bilioni,** naliomba Baraza lako tukufu kuridhia makusanyo hayo kupitia Mamlaka zao.

222. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe **TZS 5,182,89 bilioni** (Shilingi trilioni tano, bilioni mia moja themanini na mbili, milioni nane themanini na tisa), kati ya hizo **TZS 1,911.79 bilioni** zimeelekezwa kwa ajili ya kazi za kawaida, (zinajumuisha **TZS10.91 bilioni** za Mamlaka za Serikali za Mitaa na **TZS 202.61 bilioni** za taasisi za Serikali zinazojitegemea) na **TZS 3,271.11 bilioni** zimeelekezwa kwenye kutekeleza Mpango wa Maendeleo (zinajumuisha **TZS 8.03 bilioni** za Mamlaka za Serikali za Mitaa).

223. **Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.

**Dkt. Saada Mkuya Salum**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**

**Juni, 2024.**

## R. VIAMBATISHO

| | |
|---|---|
| Kiambatisho Namba 1: | Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha miezi tisa Julai – Machi 2023/2024; |
| Kiambatisho Namba2: | Matarajio ya Mapato na Matumizi Hadi Juni 2024 |
| Kiambatisho Namba 3: | Sura ya Bajeti kwa mwaka fedha 2024/2025 |
| Kiambatisho Namba 4: | Mfumo wa Bajeti kwa kipindi cha kati cha Matumizi mwaka wa fedha 2024/2025-2026/2027. |

Kiambatanisho namba 1

| UTEKELEZAJI WA BAJETI KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2023/2024 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Tarakimu ni "Bilioni" | | | |
| | Halisi Julai 2022-Machi 2023 | BAJETI 2023/2024 | BAJETI JULAI 2023 -MACHI 2024 | | | |
| MAELEZO | | | MAKADIRIO | HALISI | %BAJETI | %MIEZI 9 |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***902.57*** | ***1,419.03*** | ***1,099.76*** | ***1,075.88*** | ***75.8*** | **97.8** |
| ZRA | 449.26 | 675.60 | 535.71 | 559.34 | ***82.8*** | **104.4** |
| TRA | 323.01 | 520.64 | 386.53 | 373.17 | ***71.7*** | **96.5** |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 116.3 | 201.79 | 161.77 | 127.63 | ***63.2*** | **78.9** |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 14 | 21.00 | 15.75 | 15.75 | ***75.0*** | **100.0** |
| ***Mapato ya Washirika wa Maendeleo*** | ***180.49*** | **686.61** | **459.70** | **534.83** | ***77.9*** | **116.3** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 67.43 | 52.19 | 52.00 | 72.97 | ***139.8*** | **140.3** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.23 | 0.24 | 0.24 | 0.24 | ***100.0*** | **100.0** |
| Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 32.69 | 104.94 | 95.62 | 57.47 | ***54.8*** | **60.1** |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta | 80.14 | 529.24 | 311.84 | 404.15 | ***76.4*** | **129.6** |
| ***Mapato Mengineyo*** | ***0*** | ***717.21*** | ***630.93*** | ***596.63*** | ***83.2*** | **94.6** |
| Mkopo wa Ndani | 0 | 150.00 | 132.87 | 108.84 | ***72.6*** | **81.9** |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 0 | 567.21 | 498.05 | 487.79 | ***86.0*** | **97.9** |
| **Jumla ndogo** | **1,083.06** | **2,822.85** | **2,190.39** | **2,207.34** | ***78.2*** | **100.8** |
| Mapato yanayokusanywa na Serikali za Mitaa | 27.59 | 18.00 | 12.72 | 9.17 | ***51%*** | **72%** |
| ***Jumla Kuu*** | ***1,110.65*** | ***2,840.85*** | ***2,203.10*** | ***2,216.51*** | *78%* | 100.61 |
| **Matumizi ya Kawaida** | **731.18** | ***1,318.86*** | ***958.79*** | ***919.74*** | ***69.74*** | **95.9** |
| Mshahara Mawizara | 392.14 | 631.41 | 431.40 | 430.16 | ***68.13*** | **99.7** |
| Mshahara Ruzuku | 73.30 | 97.99 | 84.49 | 82.92 | ***84.62*** | **98.1** |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 94.25 | 236.94 | 167.24 | 131.92 | ***55.68*** | **78.9** |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 43.59 | 85.72 | 73.62 | 55.41 | ***64.63*** | **75.3** |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 127.90 | 256.00 | 202.04 | 214.96 | ***83.97*** | **106.4** |
| **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vyao** | | 10.80 | 8.00 | 4.39 | ***40.65*** | **54.9** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **299.36** | ***1,521.99*** | ***1,029.47*** | ***1,299.49*** | ***85.38*** | **126.2** |
| Fedha za Serikali | 172.27 | 742.00 | 424.00 | 562.85 | ***75.86*** | **132.7** |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund) | | 144.00 | 210.00 | 273.44 | ***189.89*** | **130.2** |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 31.84 | 99.55 | 79.63 | 57.47 | ***57.73*** | **72.2** |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta kutoka kwa Washirikawa Maendeleo | 69.22 | 529.24 | 311.84 | 404.15 | ***76.36*** | **129.6** |
| **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vyao** | **26.03** | ***7.20*** | ***4.00*** | ***1.58*** | ***21.94*** | 39.5 |
| Jumla Kuu | *1,030.54* | *2,840.85* | *1,988.26* | *2,219.23* | *78.12* | 111.6 |

**Kiambatisho Namba:2** Matarajio ya Mapato na Matumizi hadi Juni 2024

**MATARAJIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ( LIKELY OUTTURN) KWA MWAKA 20223/2024**

Tarakimu ni TZS "Bilioni"

| MAELEZO | Bajeti iliyoidhinishwa 2023/2024 | Matarajio Hadi Juni 2024 | Asilimia ya Matarajio |
|---|---|---|---|
| **A: MAPATO** | | | |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***1,419.03*** | ***1,419.58*** | **100%** |
| ZRA | 675.60 | 735.98 | 109% |
| TRA | 520.64 | 495.20 | 95% |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 201.79 | 167.39 | 83% |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.00 | 21.00 | 100% |
| ***Mapato ya Washirika wa Maendeleo*** | **686.61** | **801.36** | **117%** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 52.19 | 72.00 | 138% |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.24 | 0.24 | 100% |
| Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 104.94 | 137.12 | 131% |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta | 529.24 | 592.01 | 112% |
| ***Mapato Mengineyo*** | ***717.21*** | ***710.00*** | **99%** |
| Mkopo wa Ndani | 150.00 | 150.00 | 100% |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 567.21 | 560.00 | 99% |
| **Jumla ndogo** | **2,822.85** | **2,930.94** | **104%** |
| **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | **18.00** | 15.50 | 86% |
| ***Jumla Kuu*** | ***2,840.85*** | ***2,946.44*** | **104%** |
| **B: MATUMIZI** | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | ***1,318.86*** | ***1,311.57*** | **99%** |
| Mshahara Mawizara | 631.41 | 699.73 | 111% |
| Mshahara Ruzuku | 97.99 | 112.15 | 114% |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 236.94 | 166.90 | 70% |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 85.72 | 65.50 | 76% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 256.00 | 258.09 | 101% |
| Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani | 10.80 | 9.20 | 85% |
| **Matumizi ya Maendeleo** | ***1,514.79*** | ***1,522.98*** | **101%** |
| Fedha za Serikali | 742.00 | 608.42 | 82% |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund) | 144.00 | 275.39 | 191% |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 99.55 | 79.17 | **80%** |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta kutoka kwa Washirikawa M | 529.24 | 560.00 | **106%** |
| **Jumla Ndogo** | ***2,833.65*** | ***2,834.55*** | **100%** |
| **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vyao** | ***7.20*** | 6.30 | **88%** |
| **Jumla Kuu** | ***2,840.85*** | ***2,840.85*** | **100%** |

***Chanzo:*** *OR- Fedha na Mipango*

| Kiambatisho Namba 3 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapendekezo ya Sura ya Bajeti kwa Mwaka 2024/2025 | | | | | |
| | Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 | | | | |
| | | | | | TZS in Bilioni |
| | MAPATO | 2023/2024 | | 2024/2025 | |
| A | Mapato ya Ndani *(ikijumuisha na Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)* | | 1,437.03 | | 1,954.38 |
| 1 | Mapato ya Kodi na Non Tax | | | | 1,732.82 |
| | *(i) Mapato ya Kodi-ZRA* | 675.601 | | 845.98 | |
| | *(ii) Mapato ya Kodi -TRA* | *520.64* | | 600.08 | |
| | *(iii) Mapato yasiyokuwa ya Kodi* | *201.79* | | 265.76 | |
| | *(iv) Mapato ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE)* | *21* | | 21.00 | |
| 2 | Mapato ya Mamalaka za Serikali za Mitaa | *18* | | **18.94** | 18.94 |
| 3 | Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source) | | | **202.61** | 202.61 |
| B | Misaada na Mikopo Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | | 686.61 | | 1,516.52 |
| | *(i) Misaada wa Kibajeti (GBS)* | *52.19* | | 100 | |
| | *(ii) Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo* | *104.94* | | 322.95 | |
| | *(iii) Mikopo Nafuu ya Miradi ya Kisekta* | *529.24* | | 1,093.31 | |
| | *(iv) Mfuko wa Pamoja (Basket Fund)* | *0.24* | | 0.26 | |
| C | Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo | | 717.21 | | 1,712.00 |
| | *(i) Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo* | *567.21* | | 1,532.00 | |
| | *(ii) Mikopo ya Hati Fungani* | *150* | | 180.00 | |
| D | Mapato ya Serikali Kuu | | | | 4,961.343 |
| | JUMLA YA MAPATO (A+B+C+D) | | 2,840.85 | | 5,182.89 |
| | MATUMIZI | | | | |
| E | Matumizi Ukijumuisha (Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea) | | | | 1,911.79 |
| | Matumizi ya Kawaida | | 1,318.86 | | 1,698.27 |
| | (i) Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali | **256.00** | | **436.61** | |
| | *Malipo ya Riba za Ndani na Mitaji* | 92.00 | | 131.11 | |
| | *Matumizi mengineyo ya Mfuko Mkuu wa Serikali* | 164.00 | | 305.50 | |
| | (ii) Mshahara | **729.40** | | **893.60** | |
| | *Mshahara Mawizara* | *578.71* | | 681.18 | |
| | *Mshahara Ruzuku* | 97.99 | | 130.17 | |
| | *Michango ya Serikali katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)* | 52.70 | | *62.30* | |
| | *Mfuko wa Huduma ya Afya (ZHSF)* | | | 19.95 | |
| | *Posho la Nauli kwa Watumishi wote wa Serikali* | | | | |
| | (iii) Matumizi Mengineyo | **333.46** | | **368.07** | |
| | *Matumizi Mengineyo Mawizara* | 236.94 | | 277.76 | |
| | *Matumizi Menginiyo ya Taasisi zinazopokea Ruzuku* | *85.72* | | 90.31 | |
| | (iv)Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani | ***10.80*** | | **10.91** | 10.91 |
| | (v) Matumizi kwa Taasisi zinazojitegemea( Transfer of Expenditures) | | | **202.61** | 202.61 |
| F | Matumizi ya Maendeleo Yakijumuisha (Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea) | | | | 3,271.11 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | | 1,521.99 | | 3,263.07 |
| | *(i) Fedha za Serikali Miradi ya Kipaumbele inayoendelea* | *742.00* | | 777.76 | |
| | *(ii) Mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo* | 529.23 | | 1,093.31 | |
| | *(iii) Misaada ya Miradi ya Maendeleo* | 99.56 | | 307.76 | |
| | *(iv) Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund)* | 144.00 | | 312.00 | |
| | *(v) Miradi mipya ya Kimkakati* | | | 772.25 | |
| | *(vi) Matumizi ya Serikali za Mitaa* | 7.20 | | **8.03** | 8.03 |
| | Matumizi Serikali Kuu | | 2,840.85 | | 4,961.34 |
| | JUMLA MATUMIZI (E+F) | | | | 5,182.89 |
| | Chanzo:OR- Fedha na Mipango | | | | |

**Kiambatisho Namba** :4

| MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025-2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **Tarakimu ni TZS "bilioni"** |
| **MAELEZO** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2023/24** | **Makadirio 2024/2025** | **Makadirio 2025/2026** | **Makadirio 2026/2027** |
| **Mapato ya Ndani na Halmashauri** | **1,437.03** | **1,954.38** | **2,317.78** | **2,732.60** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,419.03** | **1,732.82** | **2,060.737** | **2,496.358** |
| Mapato ya Kodi - ZRA | 675.60 | 845.98 | 1,034.29 | 1,252.46 |
| Mapato ya Kodi - TRA | 520.64 | 600.08 | 683.51 | 826.94 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika) | 201.79 | 265.76 | 321.94 | 395.95 |
| Makusanyo ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE) | 21.000 | 21.00 | 21.00 | 21.00 |
| ***Mapato ya Halmashauri*** | ***18.000*** | ***18.94*** | ***20.76*** | ***21.99*** |
| **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer Own Source)** | | ***202.61*** | ***236.28*** | ***214.26*** |
| **Mapato ya ODA** | **686.61** | **1,516.52** | **1,941.25** | **1,525.06** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (Basket Fund) | 0.24 | 0.26 | 0.27 | 0.29 |
| Ruzuku kutoka Nje | 104.94 | 322.95 | 416.64 | 317.86 |
| Mkopo kutoka Nje | 529.24 | 1,093.31 | 1,429.34 | 1,086.91 |
| Msaada wa Kibajeti (General Budget Support) | 52.19 | 100.00 | 95.00 | 120.00 |
| **Mapato Mengineyo** | **717.21** | **1,712.00** | **1,680.00** | **1,800.00** |
| Mkopo wa Ndani (Treasury Bills/Bonds) | 150.00 | 180.00 | 180.00 | 200.00 |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 567.21 | 1,532.00 | 1,500.00 | 1,600.00 |
| ***Jumla Kuu*** | **2,840.85** | **5,182.89** | **5,939.027** | **6,057.66** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **1,318.850** | **1,911.778** | **2,555.487** | **3,013.496** |
| Mshahara Mawizara | 578.70 | 681.16 | 715.216 | 821.231 |
| Mshahara Ruzuku | 97.99 | 130.17 | 136.679 | 164.014 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 236.940 | 277.76 | 320.300 | 486.480 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 85.720 | 90.31 | 120.500 | 156.650 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 164.000 | 305.50 | 608.405 | 752.336 |
| Malipo ya Riba na Mtaji | 92.000 | 131.11 | 315.000 | 315.315 |
| Michango ya Serikali katika Mifuko ya Jamii | 52.700 | 62.30 | 68.500 | 68.569 |
| Mfuko wa Huduma ya Afya (ZHSF) | | 19.95 | 20.948 | 20.968 |
| Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani | 10.800 | 10.91 | 13.660 | 13.674 |
| Matumizi ya Uhamisho (Transfer) | - | 202.610 | 236.28 | 214.26 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **1,522.000** | **3,271.11** | **3,383.540** | **3,044.170** |
| Fedha za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 742.0 | 1,550.00 | 1,620.00 | 1,745.55 |
| Mfuko wa Kugharamia ulipaji wa Madeni ya Miradi ya Maendeleo | 144.0 | 312.00 | 324.0 | 200.0 |
| Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 628.8 | 1,401.08 | 1,429.3 | 1,086.9 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani | 7.2 | 8.03 | 10.2 | 11.7 |
| **Jumla ya Matumizi** | **2,840.850** | **5,182.89** | **5,939.027** | **6,057.666** |
| ***Chanzo: Afisi ya Rais-Fedha na Mipango*** | | | | |